**UTANGULIZI**

**NENO LA MWAKA 2025: UPAKO WA YEHOVAH NISSI – BWANA NI BENDERA YANGU YA USHINDI.**

Kulingana na Biblia katika kitabu cha Kutoka 17:13, Yehova-Nissi ni jina lililotolewa na Musa kwa madhabau aliyoijenga kusheherekea kushindwa kwa Waamaleki.

Hii ni bendera inayowakilisha uweza wake, uwepo wa ke na ulinzi juu ya watu wake. Tunapokabiliana na matatizo au changamoto katika maisha yetu, tunaweza kuinua bendera ya Jehova - Nissi na kuamini kwamba Mungu yuko pamoja nasi, akipigana vita yetu na kwa niaba yetu.

Katika maombi haya ya kufunga ya siku 28, ni maombi ambayo hatujawahi kuyafunga kwa mfungo wowote bali tumekua tukifunga maombi ya siku 21. Kwa mwaka huu 2025 hatutakua na maombi ya 7 kavu za ukamilisho badala yake tutakuwa na maombi ya siku 28, na hii ni kutokana na mafunuo amabayo Roho Mtakatifu ametupa.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Amesema katika neno lake: *1 Wakorintho 12:7 -8, Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye Yule.*

Kama tunavyojua asilimia kubwa ya watu wanafanya maombi pasipo utulivu au mpangilio na utaratibu wala muongozo,na ndio maana tumekuwa tunafanya maombi ya aina nyingi , na kwa mda mrefu tunapata matokeo madogo sana. Tulio wengi tunaomba sana mwanzoni mwa mwaka na tukimaliza maombi hayo huwa hatuna utaratibu au mfumo mwingine wa kuomba tena maombi mengine.

Hii husababisha maombi yale ya mwanzo wa mwaka kufa au kuishiwa nguvu, mwanzo wa mwaka ni kama tunachaji betri lakini ukiendelea kuitumia na usipoichaji yanaishiwa nguvu. Kwa mwaka huu tutakua na maombi mengi ya aina mbalimbali.

*Yakobo 4:3, "Hata mwaomba,wala hampati kwasababu mwaomba vibaya , ili mvitumie kwa tama zenu".*

Unapoaanza kusoma kitabu hiki cha maombi ya siku 28, ni lazima ufuate muongozo wote wa mfungo na maagizo elekezi yote yaliyolewa hapa madhabahuni katika kufunga na kuomba. Na kama ambavyo tuna neno la Unabii la mwaka huu ambalo linasema "Upako wa Jehova-Nissi, maana yake Bwana ndiye bendera yangu ya ushindi, mwaka huu kutakuwa na mapigano mengi kama ilivyokuwa wakati wa Musa sawasawa na kitabu cha "Kutoka" Musa alikua akipigana na Waamaleki, akasema kuwa Mungu atalipa kisasi kwa Waamaleki kizazi hadi kizazi na hii vita haikuishia pale kwa Waamaleki kutokana na maandiko bali hii vita ilienda kupigana mpaka kipindi cha Yesu Kristo.

Vita aliyokutana nayo Musa akiwa mtoto ndiyo vita aliyokutana nayo Yesu akiwa mtoto, kwamba watoto wote wa kiume wauwawe, ndivyo ilivyokuwa kwa Musa na Yesu Kristo. Hii inamaanisha tunaishi kwenye ulimwengu ambao una mapigano ya vita kila siku, tukiwa kama askari wa Kristo lazima tujue kwamba kila wakati ili maisha yetu yalete matokeo ya ushindi lazima tujue kuna vita, lakini kama kuna vita na hatujui kanuni ya vita ni lazima tutakua tunapigwa kila siku, ndo maana mwaka huu Mungu ametupa neno la Kinabii kwamba utakua mwaka wa Jehova-Nissi, Bendera yangu ya ushindi. Bwana wetu Yesu Kristo atakua bendera yetu ya ushindi.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Sawasawa na tawala za dunia hata kwenye siasa, tunajua Yule anayeshinda ndo bendera yake huwa inapepea, kwa mwaka huu kama ilivyo kwenye nchi yetu ni mwaka wa Siasa, mwaka wa uchaguzi na mambo mengi sana, Mungu ameniambia kuwa watoto wa Mungu waliopo ndani ya Kristo watashinda na watapeperusha bendera za ushindi wao. Maandiko yanasema "Yeyote aliyeko ndani ya Kristo bendera ya ushindi itamfunika na atashinda sawasawa na kitabu cha *Warumi 8:37, "Lakini katika mambo hayo yote tutashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda".*

*Warumi 8:17, "Na kama watoto, basi, tu warithi, warithi wa Mungu, warithi pamoja na kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate kutukuzwa naye".*

Hatutateswa tena na sisi sio watumwa wa hofu bali sisi tutamuita Baba, yani Abba Father, hivyo basi huu ni mwaka wa kupeperusha bendera ya ushindi, Mungu ameishanyanyua bendera ya Kristo Yesu kwaajili ya kupepea katika ushindi wetu.

Kupitia neno la kinabii la mwaka huu, bendera yako itainuka juu ya mlingoti na itapepea, itaonwa na mataifa katika jina la Yesu Kristo. Amen.

Ikumbukwe, ukiogopa kupoteza kwa Mungu uwe na uhakika utapoteza kwa shetani, na ukipoteza kwa shetani hakuna namna yoyote utaweza kupata msaada na kupata neema ya kukurudishia kile ulichopoteza, lakini ukiamua kuutoa mwili wako kwa Mungu na ukaomba kwa imani, ukapoteza afya, virutubisho kwenye mwili wako, nguvu, uwe na uhakika utakaporejeshewa, utarejeshewa na neema ya kupata na zaidi ya ulivyopoteza.

Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii Nikusihi uwe kama Eliya alivyoomba alijibiwa. Biblia inasema, *Yakobo 5 :16, Ungameni dhambi zenu…..* Ili maombi yako yawe na upenyo na majibu ya haraka lazima ufuate vipengele vyote vya maombi bila kujihurumia, maandiko yanasema, Mathayo 16:25, kwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake ataipoteza; na mtu atakayeipoteza nafsi yake kwaajili yangu ataiokoa.

Ukiogopa au kukwepa maombi unaharibu maisha yako mwenyewe. Mwaka huu unatakiwa kumaanisha kuomba, bora uangamie kwenye maombi ili ukiponywa maisha yako yabadilike. Nakutakia maandalizi mema ya maombi na kupitia utangulizi huu naamini yatabadilisha maisha yako.

**KWANINI TUNAFUNGA NA KUOMBA KWA SIKU 28?**

Matukio ya kibiblia yaliyorekodiwa katika Biblia yanaonesha kwamba kufunga ni kanuni muhimu katika kutembea kiroho kwa waumini.



haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Katika matukio mengi yaliyorekoddiwa ambapo watu wa Mungu wangeshiriki kufunga daima wangewashinda adui zao.

Kufunga kunaleta matokeo chanya kwa waumini wanaodhamiria kufunga kutoka moyoni na hii inahusisha kujitenga na chakula kwa kipindi flani kilichotengwa. Hii inahusisha roho, mwili na nafsi ili kuleta matokeo chanya na ushindi.

**1. Zingatia mateso ya Wana wa Israeli**

Karibu miaka 430 wana wa Israeli walikuwa katika mateso Misri. **Kutoka 3:7**, "*BWANA akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimeskia kilio chao kwasababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao.*"

Tukizingatia wana wa Israeli kukaa kule, walipofunga na kuomba ndipo Mungu aliona mateso yao, sababu kuu ya kufunga na kuomba ni ili kutoka kwenye mateso na Mungu atuone kupitia maombi haya.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**2. Zingatia Umaskini**

**Zaburi 34:6**, "*Maskini huyu alimwita Bwana akasikia, Akamwokoa na taabu zake zote*". Lengo lingine la kufunga ni kuonesha upungufu, kwamba hatuna chakula, kujishusha kuonesha kwamba tunauhitaji, kujinyenyekesha kwamba sisi ni maskini katika roho.

**3. Zingatia Adoni – Bezeki**

**Waamuzi 1:7**, "*Adoni-bezeki akasema, Wafalme sabini, waliokuwa wamekatwa vyanda vyao vya gumba vya mikono na vya miguu, waliokota chakula chao chini ya meza yangu, kama nilivyofanya mimi, Mungu amenilipa vivyo. Wakamleta Yerusalemu naye akafa kuko.*"

Kwaiyo tunaomba kwasababu kuna watu wametutesa na kutunyanyasa,na ulikua unaokota chakula chini ya meza zao kama mtumwa pamoja na hayo

wakakukata vidole gumba. Unawatumikia watu alafu wanakutesa. Hivyo ni maombi ya Mungu kukulipizia dhidi ya adui zako.

4. **Zingatia Yezebeli**

Sababu nyingine ya kuomba ni kujiokoa chini ya mkono wa uchawi wa Yezebeli. Tukizingatia namna Eliya alipewa vitisho vya kishirikiana na falme za giza, ndo maana tunafunga na kuomba ili tupate nguvu ya kiroho kuwashinda watu wa ufalme wa giza.

## SIKU YA 1: MAOMBI YA KUTENGENEZA NA MUNGU

Siku ya kwanza tutafanya maombi ya toba yaliyoambatana na shukurani. Haya ni maombi ambayo yanamgusa sana Mungu, kwasababu huwezi kuanza kumshukuru Mungu wakati una dhambi, huwezi kuanza kupaza sauti ya shukrani mbele za Mungu wakati unadhambi. Siku ya kwanza unatakiwa kutubu dhambi wewe mwenyewe alafu samehe wote ambao wamekukosea na wote unaowashikilia moyoni waite na uwasamehe na kama huwezi watangazie msamaha hukohuko walipo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Pia angalia mwili wako kama kuna kinyago au sanamu yoyote kama shanga, vitoe alafu vitakase, angalia kwenye kabati zako na za nyumbani mwenu kama kuna sanamu yoyote au kama kuna vitu umeshonea kwenye nguo, kabati za vyombo au stoo.

Kama kuna vitu vyovyote ambavyo unavyo uliishawahi kupewa na babu, bibi au waganga. Chochote kile ambacho sii cha Mungu, kinachochukua nafasi ya Mungu kwenye maisha yako unatakiwa ukiondoe.

Weka sawa vitu vyako na mawazo yako na Mungu, kama kuna chochote cha kidunia vilivyokaa kwenye maisha yako, vimeshikilia nafasi ya Mungu  na badala ya Mungu kujenga makao yake. Baada ya hapo kiri na uvitoe viteketee kwa moto wa roho mtakatifu.

***Warumi 3:23*** *“kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; “*

*usijihesabie haki, kuna mambo mengi ambayo yametuzunguka kwenye maisha ya kila siku,mwambie Mungu nisaidie mahali popote nilipokosea.

**Warumi 6:23**, "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."
Hapa unaweza ukaona kuwa hii siku ya kwanza ni siku ya kutengeneza na kumuomba Mungu asikie kutoka juu mbinguni.

**Kwanini tunaanza na maombi ya kutengeneza na Mungu kwa awamu hii?.**
Ndani ya hizi siku 5 za kwanza tutaanza na maombi ya, toba, rehema binafsi na shukrani.

Maombi ya matengenezo na Mungu yanatupa uhalali wa kuendelea na maombi tukiwa na kibali mbele zake, na haya ndo maombi yanayoleta matokeo sana.
Huwezi kwenda kwa mtu au kwa Mungu ukiwa hujatengeneza nae, lazima uwe na mahusiano mazuri nae.

Kwenye haya maombi, kama mahusiano yetu na yeye yalikatika tunayatengeneza.
Neno la Mungu katika kitabu cha **1 Yohana 3:8, "**Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi."

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Hakuna dhambi ndogo wala kubwa, dhambi ni dhambi sawasawa na, ***Warumi 3:23***, *"kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*

***Mistari ya Maombi: Zaburi 51:1, Mathayo 6:12, 1 Yohana 1:9-10, Mathayo 26:28, Yeremia 30:12,"***

**Vipengele vya maombi:**
1. Ee Bwana nisamehe kila dhambi ambayo nimefanya ninayoijua na nisiyoijua ambayo inanifanya nishindwe kufanikiwa kusonga mbele.
2. Baba katika jina la Yesu Kristo natubu na kuomba rehema kwa dhambi zangu zote ambazo nimezitenda kwa kuwaza ,kutenda na kunena ,unioshe kwa damu ya Yesu Kristo.
3. Ninasihi damu ya Yesu Kristo inene mema kwaajili maisha yangu ,nyota yangu na kazi yangu kwa jina la Yesu Kristo.

4. Ee Mungu, tusamehe kwa kuyatoa maisha yetu na vizazi vyetu kwenye madabhahu za shetani. Tuhurumie iwapo tulizifungulia milango roho za nguvu za giza za uchawi kwenye koo zetu.
5. Ninatubu kwa kujitenga na matendo yote ya kichawi na nguvu za giza ambazo mababu zetu walijihusisha nayo.
6. Ee Bwana, kwa damu ya Yesu Kristo najitenga na dhambi zote na uovu wa ukoo wangu.
7. Nakana na kujitenga na matendo yote ya kichawi, nguvu za giza na ibada ya sanamu katika jina lenye nguvu la Yesu Kristo.
8. Baba nimekukosea, nisamehe kwa kutafuta maarifa kwa roho zingine katika jina la Yesu Kristo.

**SIKU YA PILI: MAOMBI YA UTAKASO JUU YA MISINGI**

Biblia inasema kwenye kitabu cha ***Zaburi 11:3,*** *Kama misingi ikiharibika, Mwenye haki atafanya nini?*

Biblia inazungumza wazi kuwa kuna misingi ambayo tumeikuta ,aidha ya babu zetu, ya baba zetu, ya mama zetu ambayo tumeikuta, au idara flani ya ofisini, lakini waliotangulia waliishavuruga ule mfumo unapoingia unakuta mifumo imeharibika .

Usipoombea ile misingi uliyoikuta, utajikuta na wewe unapotelea pale au unashindwa kufanya vitu vizuri na mwisho wa siku unaweza ukafukuzwa kazi au ukafia hapo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Na kama unafanya kazi unaweza ukakuta labda, kila mkurugenzi huwa anafukuzwa kazi au kwenye hiyo idara kila kiongozi wa idara lazima apate kisukari au afe au kila mtu anayefanya kazi kwenye hiyo wizara lazima afukuzwe kazi kwa aibu. Usipoomba hata wewe unayefanya kazi utaishia hivyo hivyo, kwa aibu, kwa kifo au magonjwa.

Lakini pia kwenye vyanzo vyetu vya baraka, baba zetu walipata fedha na mali kwa kutumia nguvu za giza na wakaja kufa wakiwa wamepooza, usipoombea ile misingi kwa kuivunja, kuitubia na kuitakasa maana yake na wewe unasimama palepale, utaenda ila utaishia palepale, utamaliza vibaya hivyohivyo kama alivyomaliza baba yako, mama yako au mtu mwingine kwenye familia yako. Haya ni maombi ya kutakasa misingi yako.

**Mistari ya Maombi: Ezekieli 16:1-4, Luka 1:15, 2Samweli 12:11-12**

**Vipengele vya maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo kila msingi wowote wa uovu kwenye maisha yetu au maagano yaliyofanyika kwenye familia yangu, Baba naruhusu damu ya Yesu Kristo iende kutakasa na kurehemu.
2. Eh Bwana Yesu agano lolote la laana yoyote ambayo imefanyika kwenye familia yetu, juu ya maneno, juu ya matendo, naruhusu damu ya Yesu Kristo ikatakase na hiyo laana isinifwate kwa jina la Yesu Kristo, Amen.
3. Kila chanzo chochote cha kishetani cha utajiri kwenye familia yangu na mafanikio yoyote, elimu au chochote ambacho chanzo chake sii cha kiungu, ni cha shetani au cha miungu naachilia damu ya Yesu hicho chanzo kiharibike. Na mimi tangu, sasa naweka mwanzo mpya na msingi mpya katika Yesu Kristo.
4. Kwa jina la Yesu Kristo kila ulemavu wowote ambao nimerithi,unaonipunguzia kasi ya maendeleo au kasi ya kufanikiwa ndani ya Kristo.Ulemavu wowote, iwe ulemavu wa kiroho au wa kimwili,naachiliwa damu ya Yesu Kristo ikauharibu huo ulemavu kwenye maisha yangu katika jina la Yesu Kristo.
5. Eh Bwana Yesu alama yoyote iliyowekwa kwenye familia yetu kwa maagano ili kusiwepo na yoyote awe, mume au mke, mtoto, kijana au mzee akaefanikiwa kwenye umri mdogo,nafuta hiyo alama kwa damu ya Yesu Kristo.
6. Matatizo yoyote ya afya, ya uchumi, ya elimu au kwenye nyanja yoyote yanayonisubiria nikifika umri flani yaniangushe, nayafuta hayo matatizo kwa jina la Yesu Kristo.
7. Kila kafara iliyotolewa kwaajili yangu ili nisifanikiwe au nisivuke kiwango flani cha maisha flani ya kiuchumi kwenye karama na kipawa ambacho Mungu ameweka ndani yangu, hiyo kafara iteketee kwa kafara ya damu ya Yesu Kristo.
8. Kila kosa walilolifanya wazazi wangu popote mbele zako eh Mungu au mbele za Yesu Kristo kabla sijazaliwa au baada ya kuzaliwa, wazazi wangu wakiwa kwenye ndoa au kabla hawajaingia kwenye ndoa,hilo kosa nalifuta kwa damu ya Yesu Kristo, mimi sitolifanya.
9. Baba katika jina la Yesu Kristo mizizi yoyote ya uchawi kwenye familia yetu au kule nilipozaliwa upande wa Baba yangu au upande wa mama

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

yangu, nilipo oa au kuolewa, mizizi yote ya uchawi inayonifunga ili nisifanikiwe naikata hiyo mizizi kwa damu ya Yesu Kristo.

10. Kila shina lolote la uchungu ndani yangu, kwenye familia yangu,kwa watoto wangu ,hilo shina ling'olewe katika jina la Yesu Kristo. AMEN.

**SIKU YA 3**: **TOBA YA KWELI KWA AJILI YA MAKOSA YA JANA**

Kuna makosa mengi ambayo tumeyafanya huko nyuma katika nyakati zilizopita japokuwa Biblia inasema katika, 2 Wakorintho 5:17, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."

Adui zetu huwa wanatamani sana anguko letu na huwa wanatumia makosa ya jana ambayo tumeyafanya na hatukuyatubia ili kutufunga, kututesa na pengine kutuzuia na kutuchelewesha tusifikie haraka mafanikio yetu tuliyonayo.

Katika nyakati tulizo nazo tumekuwa na mambo mengi yanayojitokeza kwenye maisha yetu ikiwa ni pamoja na magonjwa ya kurithi ,kumaskini wa kurithi,laana za kurithi na mengine yanayofanana na hayo hata kwa wale waliomkiri Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yao .

Hii inatokana na makosa au dhambi za nyuma zilizotendwa ba vizazi vilivyopita au sisi wenyewe ambazo hatujazitubia hata sasa. Mbaya zaidi vizazi hivyo havikumbuki kuu ya yaliyotendwa huko nyuma ambapo inapelekea maisha yetu ya sasa kuwa magumu na mabaya japokuwa tumeokoka.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Hivyo basi ndiyo maana Roho wa Bwana amenipa ufunuo huu kwamba tunasababu kubwa ya kutubu kwaajili ya makosa ya jana tulioyatenda, tunayoyakumbuka na tusiyo yakumbuka ili Mungu apate kuonekana katika jina la Yesu Kristo.

Ndiyo maana kitabu cha, *Kutoka 20 :5-6, "inasema, Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,* nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu."

Kwa andiko hili,Mungu anapatiliza, maana yake anaadhibu na kuangalia vizazi vilivyopita.

**Mistari ya Maombi: Maombolezo 5:7, Yoshua 24:15, Yeremiah 2:5, Zaburi 79:8, Zakaria 4:14, Isaya 65:6-7**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Naita damu ya Yesu Kristo katika kila kosa au dhambi yoyote niliyowahi kuitenda huko nyuma ambayo shetani anatumia kunitesa, damu ya Yesu ipite na kuondoa hukumu ya hiyo dhambi katika Jina la Yesu Kristo.
2. Natubu kwaajili ya maovu yote na makosa yote yaliyotendwa na Baba zangu au mama zangu waliopita na waliopo yamkini waliabudu sanamu wakatoa makafala mengi,wakachinja na kumwaga damu na sadaka zingine za unga, ninairuhusu damu ya Yesu Kristo ikafute hatia zote za makosa hayo katika jina la Yesu Kristo.
3. Natubu kwaajili ya damu yoyote iliyomwagika kwaajili sadaka ili kufunga maisha yangu ya kiroho, maisha ya kimwili au maisha ya kanisa letu la Omega ambayo inadai na kushikilia ukuaji wa kanisa letu na watu wake katika jina la Yesu Kristo.
4. Ninatubu kwaajili ya Baba yangu wa kiroho, Nabii S.S Rolinga, dhambi yoyote aliyoitenda huko nyuma ama wazazi wake, wakanena maovu au mabaya ama wakatoa sadaka za aina yoyote iwe damu,fedha au unga au ya aina yoyote au yeye mwenyewe upande wake iwe baba au mama yake, au watu wa karibu yake, au makundi  ya watu waliokuwa karibu yake. Nina achilia damu ya Yesu Kristo ikaiharibu hiyo sadaka na dhambi zote za huko nyuma zinazozuiya huduma ndani yake isikue katika jina la Yesu Kristo.
5. Ninatubu kwaajili ya maovu yaliyotendwa na waasisi wa taifa letu la Tanzania waliopita naachilia damu ya Yesu ikafute kila makosa na kafara na damu zilozo mwagwa, sanamu na ibada za sanamu zilizofanyika katika taifa hili, zinazowashikilia taifa hili lisifanikiwe, lisistawi kielimu na kila nyanja katika jina la Yesu Kristo.
6. Ninatubu kwaajili ya sadaka zote zilizotolewa kwenye miungu mingine ambayo imezuiya kukuwa kwa uchumi wa taifa la Tanzania na uchumi wa vijana, uchumi wa wakulima na uchumi katika maeneo mbalimbali, naachilia damu ya Yesu Kristo, Amen.
7. Nafuta kila hati ya mashtaka, kwa damu ya Yesu Kristo iliyosimama kunishtaki mbele za Mungu ili nisifike mbali, niishie njiani au nisipige

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

hatua kwenda popote au nisifanikiwe kwenye maisha yangu, naachilia damu ya Yesu Kristo.

8. Nasimama kinyume na kila umwagaji wowote wa damu kama ilivyoandikwa katika kitabu cha **Mwanzo 9:6,** *"Atakaye mwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wa Mungu alimfanya mwanadamu.*
9. Damu ambayo imemwagwa katika taifa hili, kwenye familiia zetu, kwenye miji yetu, kwenye nyumba zetu, ambayo inapiga kelele na kudai, Eh Bwana Yesu achilia damu yako ikafute hiyo damu isiyokuwa na hatia iliyomwagika kwa jina la Yesu Kristo.

## SIKU YA 4. KUREJESHA MAHUSIANO YAKO NA ROHO MTAKATIFU

Mtu ambaye hana Roho mtakatifu, amepungukiwa na kubaki na lugha ya Roho mtakatifu, hawezi kuomba kwa bidii au kuona matokeo ya maombi yao pasipo kuomba kupitia Roho mtakatifu.Wengi wetu tumemuhuzunisha Roho mtakatifu hivyo amenyamaza na hatuoni matokeo ya uokovu wetu.
**Isaya 63:10**, "Lakini wakaasi, wakamuhuzunisha Roho yake Mtakatifu; kwa hiyo akawageukia, akawa adui, akapigana nao.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

Roho mtakatifu ni nafsi hai na inaishi bali Roho mtakatifu anaishi kwenye miili yetu, ndani yetu, anatumia miili yetu kufanya kazi, maandiko yanasema, Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu.
Unapotenda dhambi, au ukakosa ukanena vibaya ukakufuru au ukaongea vibaya ukatukana unalichafua hekalu. Roho Mtakatifu anaongea, anaskia, anahuzunuka, lakini pia Roho Mtakatifu ni rafiki wa karibu sana kuliko rafiki yako yoyote na yupo karibu sana kuliko hata nguo zetu.
Kuna hatari kubwa sana katika nyakati hizi tulizonazo kwa wakristo wengi waliompokea Roho Mtakatifu hapo awali na kunena kwa Lugha, baadae walihuzunisha na wakatenda dhambi, hivyo Roho Mtakatifu akaondoka ndani yao na wakabaki tu na lugha ya kunena kwa lugha lakini hawawezi kuona matokeo ya kuomba kwao wala majibu ya maombi yao. Nyakati tulizo nazo sasa ni za hatari sana kwasababu wengi waliopo ndani na je ya kanisa ambao wameishawahi kupokea neema ya Roho Mtakatifu huwa wanaanza kuongea uongo kwamba wameoneshwa, wamefunuliwa, wengine wanahutubu na kusema wamesemeshwa na mambo mengi kadha wa kadha

ambayo yote haya ni machukizo mbele za Roho Mtakatifu kwasababu wanakuwa hawana ushirika nae na kufunuliwa mengine yasio ya kweli ya uongo.

Maandiko yanasema tulio wengi tumemuhuzunisha Roho mtakatifu badala ya kutusaidia amegeuka kupigana nasi sawasawa na kitabu cha***, Isaya 63:10***, hivyo basi, hauwezi kuwa na ushirika na Roho Mtakatifu kama haujatubu na kutengeneza na yeye ili arudishe urafiki na ushirikiano kati yako na yeye ili yeye ndo akuongoze, kwa maana imeandikwa "Roho hutuombea kwa mzigo kusikoweza kutamkwa kwakua sisi hatujui kuomba itupasavyo, **Warumi 8 :2** , "*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba itupasavyo ,lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa*". Hivyo hatuwezi kuona matokeo yeu kama tusipokua na maombi yale ya kusihi ushirika na Roho Mtakatifu.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya Maombi: Isaya 63:10, Warumi 8:26, Matendo ya mitume 13:2, Matendo ya mitume 11:15, Matendo ya mitume 10:38, Luka 12:12.**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Eh Mungu unirehemu kwa kumhuzunisha Roho wako mtakatifu na amekuwa kinyume ndani yangu na hata ninenapo kwa lugha yake nimenena kwa mawazoea sii katika Roho wa kweli, katika jina la Yesu Kristo.
2. Eh Mungu lirehemu kanisa lako na kanisa lote laTanzania na ulimwengu mzima kwakua tumekuwa na mazoea ya kunena na kusema Roho ametuambia na kumbe sii kweli na sahihi badala yake amegeuka kupigana nasi, achilia damu yako itakase roho zetu ili tumpokee Roho wa kweli atokae kwako, katika jina la Yesu Kristo.
3. Eh Mungu wetu mwenye nguvu turehemu kwa namna tunavonena kwa lugha kwa mazoea bila kuwa na matokeo yoyote katika maisha yetu, katika jina la Yesu Kristo.
4. Eh Bwana Yesu tunarudi mbele zako kwa upya tukisihi nguvu ya Roho Mtakatifu irejee ndani yetu na uweze kunena kwa lugha kupitia Roho wa Bwana wa kweli tuliepewa anayetenda kazi katika maisha yetu kupitia huduma mbalimbali ulizoweka ndani yetu katika jina la Yesu Kristo.

5. Eh Roho Mtakatifu rudi kwa upya katika maisha yetu, tembea nasi, zungumza nasi,tupe neema ya kuomba pamoja nawe kwakua wewe ndiwe msaidizi wetu tuliyepewa utuombeae kwa mzigo kusikoweza kutamkwa katika jina la Yesu Kristo.
6. Eh Roho mtakatifu Rudisha Nguvu yako ya uponyaji, kufungua watu na kuyafanikisha yote tutendayo kwa mikono yetu na maisha yetu ya kila siku kufanikiwa kwa nguvu yako Roo Mtakatifu kupitia jina la Kristo Yesu, Amen.

**SIKU YA 5: MAOMBI YA SHUKRANI**

Haya ni maombi ya kushukuru baada ya matengenezo kati yetu na Mungu, kati yetu na Bwana wetu Yesu Kristo na kati yetu na Roho mtakatifu.

***Zaburi 103 :12,*** *"Kama mashariki ilivyombali na magharibi nivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi."*

***Isaya 43:25,*** *Mimi, naam, mimi ndimi niyafutaye makosa yako kwaajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako."*

Maombi haya ya kushukuru ambayo ni maombi ya shukrani, ni maombi ambayo yanagusa moyo wa Mungu, kwakua kipindi hiki cha matengenezo na Mungu, tunamshukuru Mungu kwakua tunaamini Mungu anaskia na anajibu kupitia matengenezo haya, kama ilivyoandikwa katika, ***Yohana 15:15,*** *"Sitawaita tena watumwa, kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu."*

Tunaamini baada ya maombi haya yote tuliyopitia ya rehema na kutubu kwaajili ya Roho Mtakatifu, tunaamini kuwa sisi sio watumwa tena bali sisi tumekua rafiki wa Bwana wetu Yesu Kristo, hivyo ndiyo maana tunamshukuru Mungu kwaajili ya mambo yote aliyotutendea.

Imeandikwa katika kitabu cha ***Zaburi 136:1***, *"Mshukuruni Bwana kwa kuwa yeye ni mwema; kwa maana fadhili zake ni za milele."*

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya Maombi: Zaburi 136 yote, Zaburi 100:4, Isaya 43 :25, 1Mambo ya Nyakati 16:8-9, Zaburi 103 :12, Isaya 12 :4-6**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo ninakushukuru kwa matendo yako makuu uliyonitendea, kwa kusamehe uovu wangu na kuyafuta makosa yangu na kurudisha uhusiano kati yangu mimi na wewe  katika jina la Yesu Kristo .
2. Ninakushukuu Mungu kwaajili ya familia yangu, kwa ujumla mke/mume, watoto, wazazi, kwa kuwalinda na kuwapigania miaka yote mpaka sasa tumeuona mwaka mpya na tunaamini tutaumaliza mwaka huu kwa ushindi katika jina la Yesu Kristo.
3. Ninakushukuru eh Mungu wa Israeli kwa maana fadhili zako ni za milele, kwaajili ya neema ya uokovu uliyonipatia kwenye maisha yangu, katika jina la Yesu Kristo.
4. Baba katika jina la Yesu Kristo, ninakushukuru kwaajili ya wazazi wangu wa kiroho, kwaajili ya kanisa langu kwa ujumla, watendakazi wenzangu, watumishi wenzangu na kila kitu kinachofanyika hapa kanisani cha maendeleo katika jina la Yesu Kristo.
5. Ninakushukuru eh Mungu uliyejaa rehema na huruma nyingi, kwaajili ya amani ya Taifa letu la Tanzania, uongozi wote na serikali, Bunge na mahakama kwaajili ya kuendelea kushikilia Nchi yetu mpaka mwaka huu, tukiamini utaendelea kuishikilia bila kuiacha kaika jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 6: USHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU**

katika nafasi na nyakati tulizo nazo wengi tumekuwa hatuna muunganiko( connection) kubwa na Roho Mtakatifu ijapokuwa tunanena kwa lugha ,tunaomba, lakini ndani ya mioyo yetu uhalisia wa Roho Mtakatifu ni kama umezimika au haupo, kwa nini ?kwa sababu roho mtakatifu hafanyi kazi na uchungu ndani ya mioyo chuki na vitu kama hivyo kwa hiyo unakuta tumebaki tu na lugha ya roho mtakatifu ambayo haina matokeo mazuri kwenye maombi yetu ,Roho Mtakatifu ni nafsi inayoishi inaongea, ina hisia ,inaumia na inafanya kila kitu ndio maana mwandishi wa kitabu cha isaya 63:10 ,anasema kwamba lakini wakaasi wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu kwa hiyo akageuka akawa adui akapigana nao.

Kwa hiyo Roho Mtakatifu unapokuwa ndani yako umehuzunisha, huwezi kuona ule upenyo na ile neema ambayo ipo ndani yake. Kwa hiyo kwa maombi pekee tunarudisha uhusiano ,anasema yeye Roho hutuombea kusikoweza kutamkwa na kitabu cha Warumi 8:26, kwa hiyo tunaomba uhusiano wake na ushirika na yeye , ikumbukwe Roho Mtakatifu haombwi bali Roho Mtakatifu unamsihi ushirika na yeye . Roho Mtakatifu ni sehemu ya mungu ambayo sisi hutupa ushindi kama yeye kwa hiyo hitaji ushirika na Roho Mtakatifu.

**Mistari ya Maombi: Isaya 63:10, Warumi 8 :26**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Ee Mungu naomba ushirika na wewe kupitia Roho wako Mtakatifu aweze kunisaidia kupata ushirika ndani yako Kristo Yesu.
2. Ee bwana yesu achilia neema kwa kanisa la Tanzania kuweza kuwa na ushirika sahihi wa maombi katika Roho Mtakatifu kwa jina la yesu kristo utuombee kwa mzigo kusikoweza kutamkwa ninaomba nguvu ya maombi ndani yangu na maombi ambayo yataleta matokeo chanya kwenye maisha yangu kwa mwaka 2025 .
3. Roho Mtakatifu, tupe udhihirisho wa nguvu za Mungu kwa kuwa wewe ndiye mtendaji mkuu wa ufalme wa Mungu katika maombi haya yetu ya mwaka huu.
4. Roho Mtakatifu rudi kwa upya kutembea nasi kama kanisa, kama mtu binafsi na familia kama ambavyo ulitembea na Yesu Kristo au ulipokuwa na Yesu Kristo alipokuwa akihubiri injili katika miji mbalimbali na kufanya kazi kubwa katika jina la Yesu Kristo.
5. Roho Mtakatifu najua wewe ni nafsi hai inayosikia, inayoumia na kuhusunika, mahali popote ambapo nilipoteza mawasiliano nawe nasihi katika maombi haya rudisha mahusiano na ushirika wangu mimi nawe katika jina la Yesu Kristo.
6. Nadhihirisha nguvu zako kwa ukubwa, ishara na miujiza kama nyakati za mitume zilizofanyika katika kipindi hiki cha nyakati za mwisho ili utukufu na heshima virudie Mungu wetu katika jina la Yesu Kristo kwa kutumia viungo vyetu.



haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 7: MOTO WA ROHO MTAKATIFU UWAKE KWENYE MAISHA YANGU**

Kama tunavyojua biblia inasema moto wa madhabahu usizimike, lakini leo tumekuwa ni washirika ambao moto wa Roho Mtakatifu umezimika. Unaweza kushangaa mtu aliokoka akiwa na moto au anatumika mwanzoni ana moto lakini baada ya muda unashangaa yule mtu amepoa. Kwa kawaida hao watumishi wa mungu walikuwa na moto wa roho mtakatifu anapanda milimani anaomba na nguvu, hii inatokana na misongo ya mambo mengi ya ulimwengu tunayopitia, Bwana Yesu kasema katika neno lake, "Ulimwenguni mnayo dhiki jipeni moyo mimi nimeushinda ulimwengu huu". Tunaishi ulimwengu wa vita ambao kama hauna nguvu ya Roho Mtakatifu na moto wake ndani yako hauwezi kuviteketeza vinavyoshindana nawe kwenye maisha yako. Kuna mambo mengi sana, kuna maisha ya utafutaji, kuna kazi maofisini, kwenye familia, ndugu, jamaa na marafiki na watu wa karibu ambao wote hawa wanaweza kusababisha kupooza moto wako ndani ya maisha yako ya kiroho lakini kama una moto wa Roho Mtakatifu hawatakupoza wewe bali wewe utawaambukiza ule moto na watakufuata wewe, kwa hiyo hii inaleta mambo mengi hata kwenye makanisa kufanyika kwa miujiza feki miujiza ya kutengeneza kwa sababu nguvu ya utendaji miujiza sahihi na moto wa Roho Mtakatifu imekauka ndani ya kanisa letu, waumini na watumishi wa Mungu.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Hivyo basi kitu pekee leo ambacho Roho Mtakatifu anasukuma hapa nchini na mahali kwingine na ndani yetu kama waumini na watumishi ili kwamba lazima nguvu ya Mungu irudi na moto wa Roho Mtakatifu urudi ndani ya kila mkristo katika kipindi hiki cha maombi hayo na kuendelea katika jina la Yesu. Biblia inasema kwamba habari za Yesu wa Nazareti jinsi mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu, naye akazunguka huku na kule akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi kwa maana Mungu alikua pamoja naye.

Moto wa Roho Mtakatifu ni uwepo wa Mungu. Tunaona Yesu alitangazwa habari zake zilienea kwa sababu alikuwa na moto wa Roho Mtakatifu. Ni moto ambao inasemekana kuna wakati mitume walitokewa na ndimi za moto zilizogawanyika uliomkalia kila mmoja, ndio maana tunaona huduma

za mitume zilikuwa ni huduma ambazo zimejawa na nguvu ya Roho Mtakatifu.

**Mistari ya Maombi: Matendo 10:38, Yohana 14:16**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Ee Bwana Yesu badilisha utambulisho wangu katika ulimwengu huu ninaoishi hapa duniani na nipe jina jipya kwa moto wa Roho Mtakatifu katika jina la Yesu Kristo.
2. Ee Bwana Yesu Kristo napokea neema ya moto wa Roho Mtakatifu ndani yangu pale ambapo nilikuwa nimepoa na kupungua ongeza na uzidishe nguvu ili niweze kushinda kila aina ya vita kwenye ulimwengu katika jina la Yesu Kristo.
3. Baba Mungu wa mbingu na nchi muweza, Baba Mungu uliyeziumba mbingu na nchi kwa Roho Mtakatifu, ambae ni Roho wako, Roho wa neema na nguvu na moto, ruhusu nguvu yako na moto wako ndani yangu uweze kuchoma na kuharibu kila nguvu ya dhambi kwenye maisha yangu katika jina la Yesu Kristo.
4. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti kama Yesu alivyokuwa na moto baada ya kutoka kwenye maombi ya siku 40 akatenda kazi njema na habari zako zikaenea katika kila kona na kando kando ya Galilaya, ninasihi ile neema na moto wake ndani yangu kwa jina la Yesu Kristo.
5. Baba katika jina la Yesu Kristo yoyote aliyejaa nguvu za shetani anayeninuia mabaya ruhusu moto wa Roho Mtakatifu uwake ndani yangu nakufuta kwa jina la Yesu Kristo
6. Kwa jina la Yesu Kristo kila hati yoyote ya mashtaka kwenye maisha yangu ambayo inasimama kunihukumu kwa maneno, imeandikwa ametupa chini mshtaki wetu, washtaki ndugu zetu na wanaosimama ili nisiweze kupokea neema na kushinda dhambi naharibu kila nguvu za yule muovu katika maisha yangu naruhusu moto Roho Mtakatifu uwake ndani yangu na kuteketeza hiyo hati ya hukumu kwa jina la Yesu Kristo.
7. Baba kwa jina la Yesu, kama ilivyo katika maandiko; ni nani awezaye kushika kaa la moto, ni nani awezaye kukuharibia moto ulao? nifanye kuwa miale ya moto na moto ulao kila nguvu za giza na ushirikina na uganga na uchawi na yote ya falme na mamlaka za giza unapo karibia

kushindana nami na kutoa mashambulizi, nisiwe wa baridi bali niwe wa moto katika jina la Yesu Kristo, muda wote Roho Mtakatifu uwake kwenye maisha yangu kuanzia sasa bila kukoma na usizimike kwa jina la Yesu Kristo, Amen.

**SIKU YA 8: KUWEKWA HURU NI HAKI YANGU KWA JINA LA YESU KRISTO**

Tunaposema kuwekwa huru ni haki yetu inamaanisha kama ilivyoandikwa kitabu cha **Yohana 8:16**

inavyosema ,basi Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli ,mwana ni Yesu Kristo ,ndio maana tunasema siku hii ya leo kwamba kuwekwa huru ni haki yangu kwa jina la Yesu, kwa sababu tumeokoka na tumefunguliwa kupitia jina la Yesu Kristo naye ametangaza tumekuwa huru, hivyo basi katika mwaka huu ninatamani sana mungu akuweke huru na ujue ni haki yako wewe kuwekwa huru kwenye kila eneo la maisha yako haijalishi ni eneo gani lazima uwepo .Swala la kuweka huru kuna kutegemea wewe mwenyewe kwamba unataka kuwa huru, ni ngumu sana kumlazimisha mfungwa awe huru mpaka pale anapotamani nakuhitaji kuwa huru ndivyo ilivyo kuokoka ni jambo moja na kumtaka kuamuru ni jambo lingine tofauti ya kuokoka na kukombolewa hivyo basi kupitia pointi ya leo jua haki yako wewe ni kuwekwa huru katika jina la Yesu Kristo.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya Maombi: Yohana 8:36, Yoeli 2:32, Yohana 8:36, Yohana 8:31**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo kama ilivyoandikwa kwamba Mwana akiweka huru na utakuwa huru kweli kweli ninaenda kinyume na kila gereza lolote familia yangu liniachia niwe huru kwa jina la Yesu Kristo.
2. Ee Mungu Baba uliyehai pigana dhidi ya maadui ndani ya familia yangu na ndani ya jamii iliyonizunguka sehemu yoyote ambayo kuna adui aliejivisha ngozi ya kondoo ndani, Baba namfichua na hasira zake nazifichwa kwa jina la Yesu Kristo.
3. Kwa jina la Yesu Kristo naruhusu kila aina ya kifungo cha gereza la dhambi yoyote, gereza la hofu, gereza la fedheha ambalo limefungamanisha maisha yangu ninaishi kwa hofu na uoga, kwa jina la Yesu, leo nawekwa huru katika jina la Yesu Kristo.

4. Kila nguvu za giza zinazo nifwatilia usiku wa manane na maisha yangu na kuyafunga, natamka kwa jina la Yesu niwe huru iniachie maisha yangu.
5. Navunja kila malango yoyote ya ufalme wa giza na magereza yote ya falme na mamlaka za giza katika familia yangu mimi sii wa kwenu tena katika jina la yesu.
6. Naachilia nguvu ya damu ya Yesu Kristo iende na ipite kwenye gereza lolote ifanye msako kwenye familia kwenye jamii niliko zaliwa au niliko lelewa, ifanye msako kwenye gereza lolote lililoshikilia hata kwa sehemu ndogo ambalo linasababisha nisiwe huru hilo gereza liteketee kwa jina la Yesu Kristo.
7. Baba kama ilivyoandikwa mwana akikuweka huru utakuwa huru kweli kweli, ninatoka kwenye kifungo chochote na gereza lolote na kama ambavyo nimewekwa huru sitafungwa tena kuanzia sasa kwa jina la Yesu Kristo,Amen.

**SIKU YA 9: KILA AMBACHO NI CHA KWANGU AU KILIKUWA NI HAKI YANGU LAZIMA NIKUPATE MWAKA HUU KWA JINA LA YESU KRISTO.**

Chochote kilichochukuliwa, kilichopotea, kilichoibiwa, unaweza ukasema na kikarejeshwe kwa jina la Yesu Kristo. Kuna watu wengi ambao tulikuwa na vitu vyetu na hatujajua kwa nini tumeibiwa, tumeibiwa miaka, tumeibiwa hatma na tumeibiwa muda ambao ni miaka, au vitu, mahusiano, elimu na mpaka tunakuja kukumbuka muda unakuwa umeenda, lakini nataka niseme jambo moja, kwamba hakuna hasara kwa Mungu kama ulipoteza miaka mitano uwe na uhakika hasara ya miaka mitano ya urejesho au kurudishiwa kilichopotea ni ahadi ya Mungu pale unapokuwa umeijua kweli.

Kwa sababu tumeijua kweli, mwaka huu chochote ambacho kilitokea hali ya hekima lazima kirudishwe kwa jina la Yesu Kristo, kwa sababu kumiliki ni haki yetu kama ambavyo bibilia inasema, "Mungu akasema tufanye mtu kwa mfano wetu kwa, sura yetu, akatawale samaki wa baharini na ndege wa angani na wanyama na nchi yote pia na kila chenye kutembea ambacho juu ya nchi" lakini shida ilianza pale ambapo mwanadamu alianza kupoteza vitu ndani nafasi yake ya maisha marefu na kila kitu, na katika kuijua kweli ambayo tuliwekwa huru basi kwa leo tumeijua kweli, naamini kila kilichopotea kitarejeshwa kwa jina la Yesu Kristo, Amen.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya Maombi: Ezekieli 39:25, Amos 9:11, Matendo ya Mitume 3:21, Isaya 61 :3-11**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai tunajua wokovu ni kitu cha thamani sana, katika **Yohana 3:16**, Bwana akamtoa Mwana wa pekee ili kila amwaminie asipotee , nguvu yoyote na maisha au chochote kilichosababisha wokovu wangu upotee ndani yangu naurejesha kwa jina la Yesu.
2. Ee Bwana Yesu najua ya kuwa toka mwanzo kuna watumishi wako wengi na watu, wanafunzi wako na waliokuwa nawe katika vipindi tofauti vya kupata na kupoteza hata mataifa, lakini waliporudia wewe uliwarudishia,ndani ya mwaka huu nipe nguvu ya kurejesha kila kilichopotea kwenye maisha yangu katika jina la Yesu .
3. Kama ilivyoandikwa kwamba mwaka huu ni mwaka wa kupeperusha bendera yangu ya ushindi ninaruhusu moto wa Roho Mtakatifu uende ukachome bendera zote za upotevu ,bendera zote zilikuwa zimepitiwa na adui zangu kwa sababu wameniteka nyara na kuninyang'anya kila kitu changu mwaka huu kila walichoninyang'anya na kiteka nyara kwa katika jina la Yesu Kristo.
4. Mahali popote ambapo maisha yangu yaliangukia au kuharibikia au yakaharibiwa na mtu yeyote natuma ni damu ya Yesu Kristo ikayakomboe na kurejesha furaha ya wokovu katika jina la Yesu Kristo.
5. Kwa jina la Yesu Kristo ninaenda kwenye ulimwengu wa roho mahali popote ambapo ameteka nyara vitu vyangu, elimu yangu, mahusiano yangu, ya watoto wangu au chochote kile kimefungiwa kuzimu natuma radi ya moto hayo magereza yakatike na kuvunjika, yaanguke yabomoke na vitu vyangu vyote virejeshwe kwenye maisha yangu kwa jina la Yesu Kristo.
6. kwa damu ya Yesu Kristo popote ambapo pamekuwa na nguvu za giza zozote zilizotushikilia kwenye ukoo au familia au uzao upande wa mama yangu au toka kijijini kwetu ambazo zimeharibu vitu vyote hatuna chochote tunachokifanya kikafanikiwa, mwaka huu natuma radi ya moto ikaangamize.
7. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila maombi ambayo nimewahi kuomba na hayajajibiwa lazima niyapate mwaka huu kwa jina la Yesu Kristo.



haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 10: Ee BWANA YESU NARUHUSU UTAWALE KILA ENEO LA MAISHA YANGU TANGU SASA**

Kama ilivyoandikwa katika Ufunuo wa Yohana 3:20 "Mimi nasimama mlangoni na kubisha hodi. Mtu akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia nyumbani kwake na kula chakula pamoja naye, naye atakula pamoja nami… Tunajua kabisa Yesu ni mtawala, anatawala mbinguni na duniani lakini halazimishi kuyatawala maisha ya mtu au kutawala kwenye maisha yako mpaka wewe mwenyewe umruhusu kutawala kwenye maisha yako.

Kuna mambo mengi sana kwenye maisha ya kawaida, kunatawala na mamlaka za falme za dunia na kuna tawala za ufalme wa Mungu ambazo ziko tawala mbili, kuna utawala wa shetani ambao mtawala wake ni shetani mwenyewe na utawala wa Mungu wetu ambaye mtawala wake anayewakilisha ni Yesu Kristo.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Kama haujawahi kuruhusu Yesu Kristo atawale maisha yako kila eneo huwezi kuona faida za wokovu wako kamili ndio maana tulio wengi leo kuna vitu vinafunguka na tunaona matokeo yake, lakini kuna vitu havifunguki mfano kuna watu wengi sana wanaweza wakaruhusu Yesu atawale maisha yao ya maombi ya kusali lakini hawezi kuruhusu Yesu atawale maisha yao ya uchumi, kwamba yeye anachokipata anagawana na Yesu Kristo.

Hivyo basi kipengele cha maombi ya kumruhusu Yesu atawale kila eneo la Maisha yako uombe kwa mzigo kwa kuugua kwamba Yesu nakubali kuanzia leo tawala maisha yangu, tawala kila kona na kila nyanja ya maisha yangu kwa jina la Yesu Kristo .

**Mistari ya maombi: Zaburi 103:1-3, Mithali 23:7, Zaburi 45:1-2, Luka 7:3-6**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo najua kwamba kuna nguvu nyingi zinazotawala huku duniani zingine zilinitawala mimi kwa mawazo kwa hisia kwa matendo lakini leo siruhusu utawala wowote wa mawazo au

matendo au mitandao ya kijamii bali ni kuanzia leo ninakata shauri Yesu Kristo tawala maisha yangu na uyabadilishe katika jina la Yesu Kristo.

2. Kwa jina la Yesu Kristo ninaruhusu damu ya mwana kondoo ipite ikafute kila maandiko yaliyoandikwa kunitawala mimi na kunitumikisha katika jina la Yesu Kristo.
3. Kwa kwa jina la Yesu Kristo adui zangu ambazo ameshaniweka katikati yao kunitawala na wananiongoza wao leo ninatoka kati yao na ninaruhusu Yesu atawale maisha yangu yote kwa jina la Yesu Kristo.
4. Kwa jina la Yesu Kristo kila uovu uliokalia utajiri wangu cheo changu ili nisiweze kukaa na kutawala na kufanikiwa naachilia damu ya Yesu Kristo ikaharibu uongofu kwa jina la Yesu.
5. Ee bwana Yesu ninashusha moto wa Roho Mtakatifu kutoka juu mbinguni uende kwenye kila misingi ya maisha yangu, Msingi ya maisha ya familia yangu na ukaharibu Kila nguvu zote za giza ambazo zinatawala maisha yetu na familia yetu katika jina la Yesu Kristo.
6. Baba katika jina la Yesu Kristo wa NazaretI kila vikao au vikundi au vyama vyovyote vya uchawi na ushirikina ambavyo vilipewa mamlaka ya kutawala maisha yangu na mawazo yangu ninaachilia moto na kuvitawanya hivyo vyama na ninatoka kati yao nitawaliwe na Yesu Kristo.
7. Kwa Jina la Yesu Kristo jina la roho iliyotumwa kunifuatilia mahali popote inapoenda napoishi au eneo lolote ambayo inapeleka taarifa kwenye utawala wa ufalme wa giza hiyo roho na hicho kifaa cha kiroho kinachonifuatilia na kiaribu kwa jina la Yesu Kristo wa nazareti amen.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

## SIKU YA 11: EH BWANA YESU NAVUNJA KILA NIRA ILIYOFUNGA FAMILIA YETU

Nira ni aina ya vifungo vibaya sana kwenye maisha ya kiroho na haikuruhusu kwenda mbali, nira inakuua, inaua elimu, inaua ndoto, inaua maono, ni kama unawekewa mipaka. Wengi wanajua nira ni mnyororo au ni kifungo au kama wale watu wanaolima kwa kutumia ng'ombe anavishwa nira na anatakiwa kwenda sawasawa na mtu anayelima anavyotaka aende, ndivyo ilivyo leo kwenye maisha yetu ya kiroho. Kama kwenye familia kuna nira hata uende Nchi gani, ufanye kazi gani, ufanye nini lakini ile nira huwa mara nyingi inavuruga maisha ya watu wengi kwa sababu huwezi kwenda zaidi

ya ulipowekewa mipaka au zaidi ya nira yenu mliyofungiwa. Sasa katika maombi haya ya siku hii kila nira yoyote ivunjike isikufunge wewe na hata kama ulikuwa ndani ya nira, hiyo nira isiendelee kukushikilia. Kitu pekee kinachoweza kuvunja nira ni mafuta ya roho mtakatifu yatakapotiwa kichwani pako au yakadondoka kwenye hiyo nira ya familia itavunjika. Mafuta ya roho mtakatifu ni nguvu ya mungu kwa roho wake mtakatifu ndio inaweza kulegeza na kukata, na kuvunja nira.

Omba kwa bidii na kwa mzigo ukiiona picha ya nira na vizuizi vingi kwenye familia yako. Katika Jina la Yesu kila nira ivunjike.

**Mistari ya Maombi: Zaburi 18:4, Isaya 9: 4 – 5, 1 Samweli 26:18-19, Wagalatia 5 :1**

**Isaya 10:27**

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Vipengele vya Maombi:**

1. Bwana Yesu Kristo uliye Bwana na mwokozi wa maisha yangu ninajua peke yangu siwezi bali kwa mkono na neema yako yote yanawezekana kila nila yeyote iliyonifunga nira za adui katika familia yangu hiyo nira ivunjike kwa jina la Yesu Kristo.
2. Kwa jina la Yesu Kristo leo ninajitenga na kila nira za familia yangu za kunifanya niwe muitaji kila iitwapo leo kwa jina la Yesu Kristo.
3. Naamuru kila nira ambayo imenifunga kutokea kwenye familia yangu isionekane au inayoonekana kwa muda mrefu inaruhusu moto wa roho mtakatifu ushuke uiangushe na kuivunja hiyo na kuiteketeza kwa jina la yesu kristo.
4. Kila mzigo niliowekewa juu yangu na kufungwa na nira shingoni mwangu kwa mafuta na moto wa Roho Mtakatifu ivunjike na mzigo uondoke mabegani mwangu niwe huru kwa jina la Yesu Kristo.
5. Nira yoyote iliyosababisha kuburuzwa na kuingizwa kifungoni katika maeneo mbalimbali ya maisha yangu mwaka huu hiyo nira iharibike kwa kutiwa mafuta ya roho mtakatifu kwa jina la Yesu Kristo.

6. Kila nira yoyote ya umaskini, magonjwa, elimu kwenye familia na kwangu hiyo nira ivunjike na haitawekwa tena kwenye vizazi vyangu vyote katika jina la Yesu Kristo.
7. Ninavunja vunja vipande vipande na kukata kata kila nila yeyote iliyosababisha nikae mahali pamoja lisitoke katika jina la yesu kristo.

## SIKU YA 12: MALANGO YOYOTE YA KUZIMU HAYATASHINDA MAISHA YANGU

Malango ni nafasi ambayo iko wazi ya hata kama malango ya baraka au heri ya

kukaa kuna malango kama ya shimo ya kumeza kile unachokipata mfano kulikuwa na lango la shimo ambapo hilo lango ndani ya shimo kulikuwa na simba wako ndani aliwekwa lakini yale malango yalipofunguliwa na danieli akaingizwa kwenye tundu la simba yale malango ya kushinda kumshinda danieli asitoke akiwa hai ,waliingizwa alipofunguliwa akaingizwa lakini yale malango vile vile hayakuwashinda kinapendekezwa kwamba wasitoke tena wakiwa hai ndivyo ilivyo leo kila malango yoyote ya kuzimu ambayo yameandaliwa mwaka huu ya kushinde kwa macho yatakachokipata ni lango linafunga linameza kila ukipata hiki lango linafunguka linameza kila ukiona kuna upenyo fulani lango linafunguka linameza mwaka huu hakuna lango la kuzimu litakalo kushinda kwa jina la yesu kristo.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya maombi**: **Mathayo 16;17-19, Isaya 54:17, Mathayo 5 :10-11**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu kila lango la ufalme wa giza linachochelewesha miujiza wangu au kumeza miujiza yangu kabla haijakamilika hilo lango lifungwe na kuteketea kwa jina la Yesu Kristo.
2. Enyi lango la kuzimu uliofunguliwa na mapepo na ufalme wa giza ili kila atakachokipata ikiharibika na kuteketea ndani yangu ndani yenu kwa mwaka huu hayo malango yenu hayatafunguka wala kufanya kazi kwa jina la Yesu Kristo.

3. Enyi malango ya kuzimu sikilizeni mna macho na masikio mnasikia yeyote anayewatumia ufungue vinywa vyenu na nafsi yenu ili kula kile ninachokipata muwe butu na mharibike kwa jina la Yesu Kristo.
4. Mamlaka yoyote ya giza iliyozingira ya maisha yangu na kufungua makanywa yake ili kumeza kilicho hai kwenye maisha yangu nafunga makanywa na mamlaka hiyo kwa jina la Yesu Kristo.
5. Kwa jina la Yesu nafungulia malango yote ya baraka iliyokuwa imefungwa kwenye maisha yangu, malango yote ya upenyo na nyota yangu mwaka huu kwa jina la Yesu Kristo
6. Kwa jina la Yesu Kristo kila lango la baraka na hazina zangu zilizofichwa mahali pa siri zilizofungiwa nafungulia hizo hazina na hilo lango zije zionekane kwenye maisha yangu kuanzia sasa kwa jina la Yesu Kristo.
7. Kwa jina la Yesu Kristo kila mjumbe wa kuzimu au wa nguvu za giza anayefuatilia maisha yangu nayapiga macho yako na kupiga mikono yako na njia zako zote ziwe utelezi hautaniona utanifuatia hautanipata kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 13:**

Maandiko yanasema kwenye kitabu kile cha **1 Samweli 17:45-46**, tunaona habari ya Daudi ambaye alikuwa ni mchungaji wa kondoo tu wa kawaida na alikuwa hana kibali hata kwa ndugu zake lakini mbele ya Daudi kulikuwa kuna ufalme, na hapakua na namna yoyote ya kuanza kutawala japo alikuwa tayari ametambulishwa na Samweli kwa kutiwa mafuta. Kwenye kitabu hicho hicho sura ile ya 16 Samweli alimtia mafuta Daudi kwamba atakuwa mfalme lakini hapakua na namna yoyote anaweza kwenda mbele baada ya kutiwa mafuta kama angekuwa hana mbinu na silaha. Tunamuona Daudi mtu aliyekuwa mbele yake alikuwa ni Goliathi ambaye alikuwa anazuia, kitendo kile baada ya Daudi kumpiga na kumuondolea kichwa Goliathi Biblia inasema ndipo Daudi akajulikana na akafanikiwa. Kwenye maisha haya ya sasa tuna watu wengi waliosimama mbele ya mafanikio yetu ambayo hatuwaoni kimwili lakini wapo kwenye ulimwengu wa roho, vingine ni vizuizi, ni maroho tu kwenye koo zetu na familia zetu tumeshatambulishwa

na Yesu Kristo na tumeokoka lakini hatuwezi kwenda mpaka tumeondoa vile vizuizi vilivyoko mbele yetu na ili kuviondoa unahitaji tu nguvu ya Mungu ya kukata na kuondoa, ukatilia mbali kila kinachojiinua mbele yetu. Bila hivyo huwezi kuona matokeo itabaki kuota ndoto na kusikia kwamba Mungu aliwahi kunionyesha nitakuwa hivi lakini hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kubadilika kwenye maisha yako mpaka umeweza kukatilia mbali watu waliosimama mbele ya baraka zako. Hivyo unapopewa nafasi ya kuomba kwenye maombi haya omba kwa mzigo mkubwa katika jina la Yesu Kristo.

Kitu chochote kinachozuia inawezekana ni dhambi, viungo, hisia, mawazo hivyo vyote ni vizuizi ambavyo vinaweza kusimama mbele ya hatima yako usipate kupata ushindi kwa hiyo sio tu kumkatilia mbali Goliathi, Goliathi alikuwa ni sehemu lakini kuna mawazo mabaya, kuna dhambi kuna vitu vingi sana, kuna viungo maana maandiko yanasema Mathayo 18 inasema kwamba “mkono ukiukosesha mwili ukate au jicho moja ni kikosi cha ling'oe kwa maana huyu mtu alikuwa yuko tayari kuondoa hata viungo vyake kuliko kukaa na viungo ambavyo vinaendelea kumzuia asifikie hatma yake katika njia yake au asifikie kile anachokiona kwenye maono yake kwamba Mungu amemweka kuwa mtu fulani kwa hiyo chochote iwe ni kwenye maisha, ndivyo ilivyo yaani huyu anazungumza kwamba hata kiungo chake yuko tayari kuking’oa lazima afikie ndoto yake ukifikia maamuzi hayo na hatua hiyo uwe na uhakika kwamba maisha yako lazima yatabadilika kwa sababu uko tayari kufanya lolote mpaka ili kuitimiza ndoto yako haya ni maombi hatari na ya vita sana ambayo unatakiwa kuyafanya katika jina la Yesu Kristo, kwa hiyo unapoomba maombi haya angalia kwamba unaweza ukashangaa unamaliza maombi kuna watu watakimbia kwenye maisha yako au kuna watu hutakutana nao tena hiyo ndio tahadhari naweza kukupa kwenye maombi haya.

haleluya.tv Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya maombi: 1 Samweli 17:45-46, Mathayo 18:8, Mithali 3:5-6, Warumi 6:12 -13, Mwanzo 19:26, Esta 8 3-7**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika Jina ka Yesu kristo kila dhambi yoyote inizongayo kwenye kiungo chochote ambayo ndio inazuia au kiungo changu chochote kwenye mwili wangu ambacho kinaungana na adui wa kimwili iwe ni mkono wewe ni mguwe ni jicho chochote kiungo changu chochote ambacho kinaungana na adui kunizuia kufikia hatima yangu kiko mbele yangu lakini kata kwa Jina la Yesu kristo na kidhoofisha kwa damu ya Yesu Kristo.
2. Kwa jina la Yesu Kristo kwa mamlaka ya uweza na nguvu ya Roho Mtakatifu kila Goliathi yeyote wa maisha yangu aliyesimama mbele yangu ili nisipite kufikia ndoto yangu na namkatilia mbali kwa jina la Yesu Kristo.
3. Kwa jina la Yesu Naman yoyote aliyekusudia kuniua ili nisipite kufikia ndoto yangu amesimama mbele yangu kwamba sitavuka lazima aniue huyo Namani kabla hajaniua na kuua ndoto yangu ninatuma radi ipige kwenye njia aliyosimama mbele yangu katika jina la Yesu Kristo.
4. Kwa moto wa Roho Mtakatifu na kwa moto ulao ninavunja vunja na kuharibu kila uchawi wowote ulioachiliwa mbele yangu kwenye malango ya upenyo wangu ili nisivuke kufanikiwa kwa jina la Yesu Kristo.
5. Kwa moto wa Roho Mtakatifu na kwa mishale na miale ya moto ulao ninatoboa toboa kila macho ya kichawi yaliyowekwa kutazama hatma yangu na fedha zangu kwamba sitafanikiwa hayo macho ng'olewe na kuharibika kwa damu ya Yesu Kristo.
6. Kwa jina la Yesu Kristo kila mwanadamu yeyote mwenye nguvu aliyetumwa kunidhoofisha imani yangu kudhoofisha hatima yangu au kudhoofisha njia yangu niendayo nayo katika Imani, huyu mwanadamu nadhoofisha hizo nguvu na peperusha kutoka kwenye njia yangu kwa jina la Yesu Kristo
7. Kila kamba yoyote iliyofungwa mbele yangu nisioweza kuikata wala kuivuka ninaruhusu moto ufurikao ukaiteketeza hiyo kamba na isionekane tena kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

8. Ee Bwana Yesu wakatilie mbali adui zangu wowote wanaosaidiana ili kuniangamiza na kunizuilia kuifikia hatima yangu katika jina la Yesu Kristo.
9. Katika jina la Yesu Kristo baba yangu baba yangu mungu mwenye uweza ambaye ni msaada kwangu nakimbilio fanya kila ngozi na nyama za adui zangu na mifupa zikauke ili wasiweze tena kuinuka kunizuia katika kile ulichoweka ndani yangu kwa jina la Yesu Kristo

**SIKU YA 14: KUSHINDA ROHO YA HOFU KWENYE MAISHA YANGU**

Biblia inasema hivi kitabu cha **Ayubu 7:14** "*ndipo unitishia hapo kwa ndoto nakuletea hofu kwa maono*"... tunaona kabisa ayubu akiwa katika ugonjwa wake ndoto alizokuwa anaota zilikuwa ni ndoto za hofu, mauti na mambo mengi sana yaliyoendana na hayo. Tulio wengi kuna watu wanateswa na hii roho ya hofu na hofu inaua ndoto zao, inaua maono yao, inaua biashara zao, mwingine anaogopa hata kuanza kitu chochote, mwingine hata kuanza elimu au kuanza kitu chochote cha maendeleo akihofia kwamba atafilisika au anaweza akaanza kisifanyike kisifanikiwe. Hali ya hofu inaua sana haraka kuliko ugonjwa wenyewe na inasababisha watu wengi wasifikie ndoto na hatima zao. Hofu ni roho kutoka kuzimu inayotumika kama silaha kubwa ya kishetani, husababisha watu wasijiamini na kumwamini Yesu Kristo ambaye amewanunua na kuwaokoa kwa damu ya thamani pale msalabani.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Ukishinda roho ya hofu utafanya mambo makubwa sana na msemo unasema usipokubali kuangamiza nafsi yako huwezi kuiokoa lakini ukikubali kuiangamiza nafsi yako ndipo utakapoiokoa unaendana na msemo wa wafanyabiashara wanaosema if you don't take risk huwezi kufanikiwa usipokubali kujitoa mhanga leo au katika maombi haya ya kushindana na kuishinda roho ya hofu na kuiondoa lazima ninaamini ni roho ikiondoka mwaka huu utafanya mambo makubwa sana kuliko ambao uliwahi kufanya miaka mingine katika jina la Yesu Kristo.

**Mistari ya maombi: Zaburi 27:1-3, 2 Timotheo 1:7, Isaya 54:17, Yakobo 4:7**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Eh Yesu Kristo Bwana na mwokozi wa maisha yangu kama ulivyoniokoa katika dhambi ndivyo hivyo ninaomba uniokoe katika roho hii ya hofu kwa jina la Yesu Kristo
2. Uliyeachiliwa kutokea kwenye familia yangu au kutokea mahali nilipozaliwa kusoma unayepigana na kushindana na maisha yangu achia maisha yangu kuanzia sasa kwa jina la Yesu Kristo
3. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti nakataa uoga wa aina yoyote, uoga wa Maisha, uoga wa kifo, uoga wa kujaribu kufanya chochote cha maendeleo bali Ee Mungu achilia roho ya ujasiri ndani yangu kwa jina la Yesu Kristo
4. Katika jina la Yesu Kristo n navunja kila agano lolote la uovu lililo fanyika kututia hofu maishani mwetu katika jina la Yesu Kristo
5. Kwa jina la Yesu Kristo navunja kila aina yoyote ya utumwa wa uoga utumwa wa dhambi na uoga kwenye maisha yangu ninayosababisha nisifanikiwe kwa jina la Yesu Kristo
6. Kwa jina la Yesu Kristo kila roho yoyote inayoleta hofu ikasababisha magonjwa mateso msongo wa mawazo na mambo yote yanayoambatana na hayo, naing'oa ndani yangu kwa jina la Yesu Kristo
7. Baba katika jina la Yesu Kristo kila ndoto mbaya zozote ninazoota na kuniletea hofu sana hizo ndoto zipotee kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 15: KUVUNJA KILA ROHO YA VIAMBATA VYA FAMILIA**

Tunaona kumekuwa na changamoto kubwa kwenye familia zetu tuna roho inaitwa roho ya kufanana kwenye familia nzima unakuta kama mtu alivyokufa baba yake ndivyo anavyokufa yeye alivyo shindwa *mama yake ndivyo anavyoshindwa yeye. Kitabu kile cha* ***Ezekiel 16:44*** *"kama alivyo mama ndivyo alivyo bintiye"* kwa hiyo tunaiona kabisa ni roho ambayo inafanya kazi sana kwenye familia, yaani mnafanana kila kitu unakuta watu kwenye familia nzima wanafanana kama ni watoto wa kike wote wana vitu na Maisha ya kufanana. kama ni namna yoyote ya muonekano wake aliyesoma anafanana hivyo hivyo maisha yake ni yale yale ata ambaye hajasoma ni yale yale bibilia inasema kitabu cha kutoka kwamba wana wa

israel walipougua kwa ajili ya utumwa wao Mungu akasikia kutoka mbinguni akamtuma mtu kwa hiyo kura yao ilikuwa inafanana kutembea yao ishi yao yote ilikuwa inafanana sasa kuna familia fulani unakuta maisha yenu wote mnafanana yaani mnafanana maovu aina ya uovu yaani unakuta wote mnafanana eh kutokuoa kuchelewa kuolewa kuchelewa kuzaa yaani vitu vinafanana , aliyesoma na ambaye hajasoma wote maisha yanafanana. Hii ni roho mbaya sana inaitwa Viambata vya familia wote mnafanana. Katika maombi haya ya siku hii ya leo lazima iwe viambata vya familia viishe na viteketekwa jina la Yesu Kristo haijalishi mnafanana nini wewe lazima ujitenge na hayo mazoea ya roho za kufanana iishe kwa Jina la Yesu Kristo.

Kuna watu viambata vya familia haviwezi kuwa kwenye mabaya tu ingawa hapa tunashughulikia na mabaya lakini inaweza ikawa kwenye mema. Lazima tuombe Mungu atupe viambata vya familia vya mema ndio vitufuate ila vile vya mabaya visitufuate kama ambavyo kitabu cha ***2 Wafalme 14:3*** “*akafanya yaliyo mema machoni pa bwana ila si kama babaye daudi akafanya kama yote aliyoyafanya babaye yoashi*”, umeona anasema akafanya yaliyo mema kwa hiyo kuna roho ya viambata vya familia ya upande wa mema na kuna roho ya viambata vya familia ya upande wa mabaya wewe kwenye maombi yako leo omba kwamba Mungu avunje kila roho yaviambata vya familia ya mabaya na yale mema ya kufuate wewe kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya Maombi; Zaburi 118:17, Zaburi 91:14, Isaya 9:19,Isaya 54:14-15**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo kila roho ya mazoea ya tabia zozote za dhambi au kushindwa kwenye familia yangu kata mawasiliano na najitenga nayo kwa jina la Yesu Kristo
2. Kila nguvu inayo nivuta kuelekea kwenye kuchanganyikiwa na kushindwa kufanya kazi na kufanikiwa ambako wamekuwa nako wengine kwenye familia yangu ninajitenga kwa jina la Yesu Kristo
3. Baba katika jina la Yesu kila roho za kufanana kwenye familia zetu, kufanana kwenye Maisha, elimu, Uchumi, hali ya kindoa na namna

yoyote ya kufanana mimi sitafanana nao na kizazi changu kwa jina la Yesu Kristo

4. Baba katika jina la Yesu Kristo shusha moto wako Roho Mtakatifu ukateketeza kila chanzo kinachosababisha familia yetu wote tufanane maisha kwa jina la Yesu Kristo aliye hai
5. Baba katika jina la Yesu Kristo kila jaribio lolote la kishetani ambalo linafanyika kutujaribu kutuua kabla hatujatimiza ndoto zetu hilo jaribio liharibike na hiyo roho ivunjike kwa jina la Yesu Kristo
6. Baba katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti kila mkataba wowote uliowekwa kwenye familia zetu na nguvu za giza au wakina yesu abeli wa ukoo na familia zetu huo mkataba nina uharibu na kuteketeza kwenye moto wa roho mtakatifu
7. Kwa jina la Yesu kila ngome yoyote ya kifo na maafa yoyote kwenye familia zetu ambazo zinawaua watu wenye ndoto kubwa na ambao wamewekwa kitu kikubwa cha kimungu ndani yao hizo ngome ziharibike na kuteketea zisionekane tena mahala pake kwa jina la Yesu Kristo
8. Baba katika jina la Yesu Kristo kila roho yoyote ya mazoea ya uvivu ambayo inasababisha hofu ya kujaribu kufanya jambo lolote la maendeleo kwenye familia yetu hiyo roho ivunjike na kuharibika kwa jina la Yesu Kristo

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

## SIKU YA 16: KUKATA MINYORORO INAYOTUUNGANISHA KUFANANA KIMAISHA

Biblia inasema kwamba tunawona wakina Petro wakati wa Herode biblia inasema wakati katika watu wanne askari wa nne na wakafungwa minyororo hii ni dhahiri kwamba kuna watu wengi sana ambao ufalme wa giza au maagano na kwenye koo zetu yametuweka chini ya uangalizi chini ya ulinzi wa askari wa kiroho hasa askari wa ulimwengu wa giza au askari wa kwenye ukoo kama miungu mizimu mapepo na maagano kulinda kwamba hawa watu hata kama wataenda wapi wasifanikiwe kwa hiyo imefunga ni kama unahisi unatembea kwenye zaburi inasema na tuvikate vifungo vyao

na kukata mapigo yao ya chuma na minyororo ya chuma, kwa hiyo unaweza ukawa unaishi unatembea unafanya kazi unakula unakunywa lakini kwenye ulimwengu wa roho kuna minyororo ambayo imeshikilia maisha yako yaani huwezi kwenda mbali kimaisha hata kama umesoma maisha yako yanafanana na wale ambao hawajasoma kwenye familia yako hata kama una fedha lakini maisha yako na kula yako hauwezi kula tofauti na wale ambao kwenye familia yenu hawana fedha. Wanaweza wakawa wana fedha lakini shetani akaleta magonjwa ambayo yakakuzuia  aina fulani ya vyakula usiweze kula lengo anataka kukupeleke kwenye mfumo wa aina ile ile ya kula wanayokula wengine ambao hawana chochote kwenye familia. Leo hii tunaenda kuikata ile minyororo, unayoijua ama huijui lazima ivunjike na ujitenge kabisa. Hizi ni chain spirit, ni roho za mfanano ni ile minyororo inawaunganisha inawafunga bila wewe kujua kwa sababu hata Petro alipokuwa amefungwa Bibilia inasema akalala usingizi na amefungwa lakini analala hana uwezo wa kufanya lolote, kama kanisa lisingeomba Petro isingeondoka na akapata ufahamu wa kutoka nje bila kuambiwa na malaika toka nje kwa hiyo unaweza ukawa umefungwa minyororo au umefungwa vifungo fulani bila kufanana na familia yako lakini uko tu sawa unalala tu usingizi huoni shida yoyote ni mpaka upate msaada wa Mungu wa kiroho. Roho wa Mungu akushtue kupitia malaika zake kwamba amka toka akutoe nje ndio uone nuru kwamba anatakiwa kufunguliwa kwa kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Misatri ya maombi: Zaburi 2:3, Isaya 52:2, 2 Nyakati 33:11, Marko 5:4, Matendo 12 :6-7**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo kila nguvu yoyote ile ambayo imenifunga bila mimi kujua ili nifanane na watu wa familia yangu hiyo nguvu ivunjike kwa jina la Yesu Kristo.
2. Kwa jina la Yesu Kristo kwa maana imeandikwa tutavipasua vifungo vyao na kukata minyororo yao kila kifungo kilichofunga ufahamu akili au

maisha na minyororo iliyonifunga kwa siri kwa muda mrefu kuanzia sasa hiyo minyororo iteketee kwa moto wa Roho mtakatifu

3. katika jina la yesu kristo baba yangu simama umzamishe kila farao yeyote wa ukoo wetu ambaye ameyafunga maisha yetu sehemu moja na kututeka mateka katika jina la Yesu Kristo.
4. Kila adui anayesubiri kushangilia matatizo yangu au kushangilia mateso yangu mahali popote ambapo pameshika maisha yangu na kufunga kwa siri tukafichwa wote watoto wa kiume au wa kike tunafanana kuanzia sasa hiyo minyororo ikatike na isiende kwa watoto wangu kwa jina la Yesu Kristo
5. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila minyororo iliyotukusanya na kutuweka kwenye magereza na kuwatuwekea ulinzi ili tusifunguliwe na kutoka kwanza nalibomoa hilo gereza na minyororo hiyo katika yenyewe kwa moto wa roho mtakatifu katika jina la Yesu Kristo

**SIKU YA 17: KILA UTAWALA WA ROHO ZA UMASKINI IWE MWISHO TANGU SASAk**

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Roho ya umaskini ni roho kabisa inayotawala na usipoishughulikia inafanyaga kazi bila aibu haijalishi wewe umesoma au hujasoma una biashara au hauna, una ufahamu au hauna, una uwezo mkubwa au hauna. Kuna watu wengi sana wana uwezo mkubwa wa kibiashara na fikra lakini wamefungwa ndio maana unaweza ukashangaa mtu akiwa amesoma anafanya kazi serikalini au ameajiriwa au anafanya kazi kwenye mashirika makubwa duniani anaweza akawa ana fedha lakini wakashangaa wakati anamalizika kwenye ule umri wa uzee unashangaa inapata janga kubwa pengine la ugonjwa linakula hela zote anaishia, yaani anabaki maskini kama hajawahi kuwa Tajiri. Mwingine unakuta ile anastaafu anapata tatizo au miaka michache kabla ya kustaafu anapata skendo anapata kesi hata ya hujumu Uchumi, inasababisha mali zake zote kutaifishwa anarudi kuwa sufuri. Sasa tuangalie roho ya umaskini kufanya kazi kwenye maisha ya kati tunaangalia hii roho ya umaskini inafanya kazi mwisho haijalishi umeajiriwa au umefanyaje kuna watu wengi sana walikuwa na fedha nyingi lakini ghafla wamekufa wakiwa maskini hawana ata pa kulala kuna wengine walikuwa na majina makubwa kwenye matatizo makubwa duniani wamefanya kazi lakini cha ajabu anaondoka familia yake inarudi kwenye umaskini mkubwa kuliko

ambavyo aliwahi kuwa nao. Kwa hiyo kumbe ni zile roho huwa zinaweza kukuacha ukaenda mwisho wa siku zinakuja kukupiga wakati wa umaliziaji wako ndio maana bibilia inasema Yesu alifanyika laana na akafanyika masikini sisi tupate kuwa matajiri wa ulimwengu huu. Kusudi na mpango wa Mungu ni kwamba Yesu alimalizia pale msalabani katika hali ya umaskini ili sisi tumalizike kwenye maisha yako ya duniani katika utajiri na utukufu wa Yesu Kristo. Mwambie mungu akupe mwisho mwema nizifie kwenye umaskini wa roho na umaskini wa mwili vyote viishe ili upate utajiri wa roho yako na utajiri wa mwili wako katika jina la Yesu Kristo.

**Mistari ya maombi: 1 Sam 2:7-8, Yohana 5:15-16, Zaburi 9:18, Zab 12:5, Zaburi 22; 26**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo naamuru kila laana ya mababu inayonitakia umaskini maishani mwangu ili nife nikiwa maskini hiyo laana iteketee juu yangu na kizazi changu chote kwa jina la Yesu Kristo.
2. Eeh Bwana Mungu kama ilivyoandikwa katika kitabu cha kumbukumbu la torati kama ipapo utaiweka kwamba ni wewe mungu utupaye nguvu ya kupata utajiri ili ufanye agano letu sisi nawe ikiwa imara naomba uachilie nguvu ya kupata utajiri kwenye maisha yangu na kizazi changu kwa jina la Yesu Kristo
3. Baba katika jina la Yesu sikia kilio changu na uondoe kila laana ya umaskini ambao nimeikuta nilikozaliwa kwenye ukoo wangu na familia yangu mimi nifanye kuwa tofauti kwa utukufu wa jina lako Yesu Kristo
4. Katika jina lako Yesu Kristo umesema katika neno lako mwanao Yesu Kristo alifanyika maskini japokuwa alikuwa tajiri hii sisi tupate kuwa matajiri kwa umaskini wake kila roho ya umaskini kwenye ukoo wangu na familia yangu sio fungu langu na kizazi change.
5. Kwa jina la Yesu Kristo medali na kila agano lililoandikwa na walinzi wa kipepo waliowekwa kwenye familia yangu ili asiwepo yeyote atakaye kufa au kumaliza maisha hapa duniani akiwa tajiri hilo agano lilivunjike kwa jina la Yesu Kristo
6. Kwa damu ya Yesu Kristo funika kila funiko kila mfuniko wowote uliotufunika kwenye ukoo wetu ili wote tuishie kwenye maisha ya

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

mateso na umaskini hilo funiko liteketezwe kwa moto wa Roho Mtakatifu.
7. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila chungu chochote kilichowekwa majina yetu kinachopikwa na kuchemka ili wote tuishie kwenye maisha ya mateso na umaskini hicho chungu kipasuke na kubomoka kwa jina la Yesu Kristo

**SIKU YA 18: KUHUWISHA NDOA YANGU/NDOA YANGU HAITAVUNJIKA KAMA ZA WENGINE BALI IWE HAI**

Hiki kipengele cha ndoa ni changamoto kubwa sana tulizonazo katika kizazi hiki tulicho nacho. Ndoa ni taasisi ambayo ilianzishwa na Mungu kwenye bustani ya Eden, kwa hiyo kama tunavyojua kwamba shetani anapambana na Mungu kuonyesha kile alichokifanya Mungu yeye anaweza kukiaribu na ndio maana leo tunaona wimbi kubwa sana la ndoa za watu maarufu, watu wa kawaida, wafanyabiashara, hata watumishi wa Mungu zimeingia kwenye changamoto kubwa sana za kuvunjika na kukosa nguvu, afya, hata walioko ndani ya hizo ndoa wana migogoro mikubwa na hazina afya yoyote.

Sawa sawa na andiko la **Mwanzo 2:18,** *"Mungu akaona si vyema mtu huyu awe pekee yake bali atamfanyia msaidizi wa kufanana naye".* Maanake ndoa ni mpango wa Mungu wa baraka na ndio maana Biblia inasema kwenye kitabu cha Mithali "apataye mke apata kitu chema naye ajipatia kibali mbele za Bwana". Leo hii adui amezipiga ndoa na kupigwa kwa ndoa ni kusababisha familia zisiwe na nguvu ya kwenda mbele na kufanikiwa katika mambo yote, ndoa ikishapigwa uchumi unapigwa, watoto wanasambaratika, tunapata watoto wa mitaani na tunakosa maadili ya kulea watoto wetu. Kila ndoa inayochechemea usijihesabie haki na unapoona ndoa yako bado iko vizuri usiseme ombi alinihusu hakuna mtu unatakiwa kuomba sana kama wewe ambaye bado ndoa yako iko sawa maana adui anaiwinda sana kuliko yule ambaye ndoa yake imeshaonekana tatizo. Ni rahisi sana kutibu ugonjwa ambao tayari umeonekana nje kuliko ule ugonjwa ambao haujaujulikana unaokula mtu ndani. Kwa wewe ndoa yako ambayo iko vizuri, bado mnapendana, mnasikilizana unatakiwa kuomba sana kuliko yule ambaye matatizo ya ndoa yameshaonekana kwa sababu ni rahisi kuyatibu.

**Mistari ya maombi: Mwanzo 2:18,21-25, Mathayo 19:1-9, 1 Wakorinto 7:27, Malaki 2:14-16, Mithali 14:1 ,31:10 -12**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Ee Bwana yesu ingilia kati ndoa yangu na ulete mabadiliko chanya kwenye ndoa yangu kama kuna mpango wowote ambao tayari umeanza kuibuka wa kuvunja ndoa yangu huo mpango uteketee kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti.
2. Bwana Yesu kwa maana imeandikwa si vyema mtu huyu awe pekee yake bado utamfanyia msaidizi kila roho ambayo inapiga msaidizi wangu asiweze kuwa upande wangu na kujenga familia iwe ni roho ya ukoo wake au familia yake hiyo roho iteketee haitamgusa mume wangu au mke katika jina la Yesu Kristo
3. Baba katika jina la Yesu Kristo kila mapepo yanayoondoa mvuto wa ndoa yangu kwa mwenzi wangu mume au mke na kuondoa ile raha ya kufurahia ndoa yetu hayo mapepo ya mizimu majini mahaba yateketee yote kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti
4. Baba katika jina la Yesu Kristo ninawaua wanaume wakipepo majini mahaba yanayomvamia mume wangu au mke wangu ili kutuondolea furaha ya tendo la ndoa kwenye maisha yetu katika jina la Yesu Kristo
5. Baba katika jina la Yesu Kristo kila mwanaume aliyewahi aliyetangulia kumuoa mke wangu kabla mimi sijamuoa au mwanamke aliyetangulia kuoana na mume wangu kabla mimi hajanioa ambaye ndio anaongoza maisha yake ili mimi ndoa yangu ya kimwili ikose furaha na amani huyo mwanaume au mwanamke namuua ateketee na hiyo ndoa anaivunja kwa jina la Yesu Kristo
6. Baba katika jina la Yesu naamuru moto kutoka juu mbinguni iwateketeze makahaba wote wa kiroho na kimwili wa kike ama wa kiume wanaonyemelea kuvunja ndoa yangu katika jina la Yesu Kristo
7. Baba katika jina la Yesu Kristo ninapulizia damu ya yesu kwenye ndoa yangu haitavunjika wala kuvurugika na watoto wangu hawataacha kuolewa wala kuoa madhabahuni katika jina la Yesu Kristo, Amen

**SIKU YA 19: TUMBO LANGU LAZIMA LIWE NA UZAZI, HAKUNA TENA KUTOKUZAA**



haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Changamoto kubwa ambayo tunayo katika kizazi hiki tumegundua wanawake wengi mambo ya uzazi yamekuwa ni changamoto lakini hapa napongelea tumbo langu lazima liwe na uzazi siongelei tu kwa habari ya uzazi wa kuzaa watoto kama wamama wanavyobeba mimba na kuzaa Watoto, bali naongelea tumbo la uzazi hata kwenye maisha yetu ya kawaida kwamba kile unachokifanya kiweze kuzaa. Mwaka huu 2025 lazima kila utakachokipanda kama mbegu kwenye biashara, kwenye elimu, kwenye uzazi, au mahali popote lazima kizae. Tulio wengi tumetumia nguvu kubwa sana kufanya uwekezaji kama mbegu za uzazi ili tuweze kuvuna matunda kama watoto lakini mwisho wa siku tuna kuta tunapata hasara. Kwenye maombi ya leo msihi Mungu lazima matumbo yetu ya uzazi yazae na yalete matokeo ijapokuwa mistari inaweza ikaonyesha kuonyesha matumbo ya uzazi zaidi ya kimwili lakini tunalenga uzazi wa pande zote mbili.

**Mistari ya maombi: Kutoka 23:26, 1 Sam 1:1-20, Zaburi 127:3-5, Zaburi 144:12, Zaburi 92:12, Mwanzo 18:14**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila mishale ya uzazi ambayo inapiga tumbo langu la uzazi nisiweze kuzaa watoto wa kimwili au watoto wa mafanikio ya kiroho, ninaizima hiyo mishale kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti
2. Baba katika jina la Yesu Kristo kila agano lililowekwa kwenye familia yetu kwamba hakuna mtu atakayezaa watoto wakaishi au atakayeanzisha kitu kikazalishwa ninaijua hilo agano nalivunja kwa jina la Yesu Kristo
3. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila maadui wa uzazi wangu wanaosubiria nini wanaonisubiria hili ni dhahabu wa mle mtoto na kumwangamiza hii nikianzisha kitu kiharibike au maadui wateketee kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti
4. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila sauti ya ugumba inayopiga kelele kwamba huyu hatazaa hatafanikiwa na wakatamka na laana au akizaa watoto wafe hiyo sauti naizimisha kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti
5. Baba katika jina la Yesu Kristo kila pandikizo la nguvu za giza lililoingizwa kwenye tumbo la uzazi la mke wangu au uliyoingizwa kwenye tumbo la uzazi na kazi za mikono yangu hilo pandikizi na ling'oa kwa jina la Yesu Kristo na halitapandikizwa tena

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

6. Baba katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti kila matamko yaliyotamkwa ya laana na yakatolewa sadaka kwamba hakuna mtu yeyote ataanzia chochote na kuzaa kwenye familia nayafuta hayo matamko kwa jina la Yesu Kristo
7. Kila agano la kwenye familia zetu kwa watoto wa kike au wa kiume kwamba kila yeyote anayebeba mimba ziharibike kabla ya wakati au anaianzisha kitu chochote kiharibike kabla hajaanza kupata faida hilo agano livunjike kwa jina la Yesu Kristo
8. Baba katika jina la Yesu Kristo yeyote yule alienda njia panda akafanya uchawi na uganga ili kufunga matumbo ya uzazi tumbo la uzazi la mke wangu au kufunga kiuno cha uzazi cha mume wangu kwa jina la Yesu Kristo, hilo agano lililofanyika njia panda nasababisha hiyo njia panda ivunjikevunjike na kuharibika kwa jina la Yesu Kristo
9. Katika jina la Yesu Kristo chochote kilichodumaa uliodumaza uzao wangu wakadumaza elimu zao kuanzia sasa na chipusha katika jina la Yesu Kristo

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 20: KILA ROHO YA URITHI NA MAOVU KWA MZALIWA WANGU WA KWANZA LAZIMA IANGAMIE**

Wazaliwa wa kwanza ni watu ambao wamekuwa na vita kubwa sana kwenye familia hizi za kwetu, kwa sababu wao wanafanyika kama lango. Katika kitabu cha **Zaburi 24:7-10,** "*Inueni vichwa vyenu enyi malango mfalme wa utukufu apate kuingia nasema ni nani huyo mfalme wa utukufu unasema bwana Hodari, Bwana mwenye nguvu Bwana wa majeshi*". Sasa wazaliwa wengi wa kwanza ni malango na akipigwa mzaliwa wa kwanza unashangaa watoto wote wanapigwa, ikitokea mzaliwa wa kwanza amebeba mimba utashangaa watoto wote wanabebea mimba nyumbani. Ikiwa mzaliwa wa kwanza amepitia changamoto na wote wanakita hivyo kwa sababu wao ni lango na kazi kubwa ndio maana tunamuona reuben alienda kufunga lango mpaka akalala na mke na masulia wa baba yake na akapata laana umeona kwa hiyo wazaliwa wangu wa kwanza kumkuta ni changamoto kubwa sana ambazo zinapitia ili uweze kumkomboa mzaliwa wako wa kwanza lazima utumie kanuni iliyotumika wakati wa Yesu ndio alikuwa mzaliwa wa kwanza lakini kanuni yake ni kwamba iliyotumika kwamba Yesu alitamkiwa mema tangu hajawa tumboni kwa mama yake na biblia inasema sisi wazaliwa wa kwanza wa takatifu juu mbinguni, kwa hiyo

lazima uanze kumtenga mtoto wako kwamba yeye mzaliwa wangu wa kwanza atakuwa kama wazaliwa wa kwanza wa ukoo wangu na unakuta wanafungwa wazazi wengi wa kwanza wanapata shida ya kuumwa na vichwa au vipanda uso hii ni kwa sababu wao ni vichwa kwenye malango ya wazazi wao au malango ya kwenye familia. Kwa hiyo lazima unapoona una changamoto kubwa ya kuumwa kichwa kama mzaliwa wa kwanza lazima uanze kupiga roho za mizimu mizimu ya ukoo ndio inawafuatia sana wazaliwa wa kwanza tabia za kurithi matatizo ya kurithi magonjwa ya kurithi ya kufanana yanamfuata sana wazaliwa wa kwanza.

Kwa hiyo kama wewe ni mzaliwa wa kwanza au mtoto wako amezaliwa kwanza mtenge sana na maroho ya uovu, madhabahu za uovu, kushangaa mzaliwa wa kwanza anaanza kuvuta bangi, mzaliwa wa kwanza anafanya vitendo yaani ulevi wazaliwa wengi wa kwanza unaingia kwenye vitendo viovu kupitia prayer pointi hii mzaliwa wako wa kwanza ataingia kwenye vitendo viovu kwa jina la Yesu Kristo

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya maombi: Hesabu 3:40-51, Kutoka 13 :2,12, Hesabu 14 :18, Isaya 15:4-9, Mwanzo 27:18-20**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo najivua kila laana na urithi muovu wa mababu zangu kama mzaliwa wa kwanza au kwa wazaliwa wangu wa kwanza kwa jina la Yesu Kristo nyingine kwa jina la Yesu Kristo ewe mfumo mwovu wa kutokufanikiwa kwa wazaliwa wa kwanza kwenye ukoo wetu na familia zetu kwa watoto wangu na jamii yangu huo mfumo uvunjike na usiendelee kwa jina la Yesu Kristo
2. Kila madhabahu ovu za familia zinazofuatilia maisha yangu kama mzaliwa wa kwanza au kwa wazaliwa wangu wa kwanza hizo madhabahu ziteketee na kuangamia kwa moto wa Roho Mtakatifu katika jina la Yesu Kristo
3. Kila laana yoyote ya familia zinazo warithisha maisha wazaliwa wangu wa kwanza na familia zao au na familia yangu hiyo laana ivunjike kwa wazaliwa wangu wa kwanza kwa jina la Yesu Kristo
4. Kila vita na vurugu zozote za kurithi kwenye maisha ya wazaliwa wangu wa kwanza au wazaliwa wetu wa kwanza mahali popote ambapo

zimewekewa au zimetengenezwa tunateketeza na kupeleka moto wa roho mtakatifu kwa jina la Yesu Kristo

5. Baba katika jina la Yesu Kristo kila magonjwa ya kurithi au tabia ya hofu za kurithi kama vile ulevi uzinzi uasherati wizi na namna zozote za maovu kuabudu miungu mingine kwa wazazi wako wangu wa kwanza nawatenga na hizo roho kwa jina la Yesu Kristo
6. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila muunganiko wowote wa dhambi za kurithi kwenye koo zetu kupitia wazaliwa wa kwanza na matatizo na tabia za kurithi na kata mawasiliano na hazitaunganisha watoto wangu kwa jina la yesu Kristo
7. Baba katika jina la Yesu Kristo ninawaweka huru kutoka kwenye aina yoyote ya vifungo vya familia zetu wazaliwa wangu wa kwanza wote kwa jina la Yesu Kristo
8. Baba katika jina la Yesu Kristo madhabahu ya familia au nyumbani mwa baba yangu au mama yangu ambazo zinawafuatilia wazaliwa wetu wa kwanza na kuwafanyia na kuwatendesha matendo maovu hizo madhabahu ziteketee zote kwa jina la Yesu Kristo
9. Baba katika jina la Yesu Kristo kila madhabahu zilizojengwa chini ya maji au kwenye milima au njia panda au kwenye koo na miti yoyote yale maiti makubwa zile ya shela na zikata hizo ashera na kuzivunja hizo madhabahu popote zilipo hazitawafuatilia watoto wangu na wazaliwa wangu wa kwanza kwa jina la Yesu Kristo
10. Baba katika jina la Yesu Kristo nafuta jina langu na majina yote ya watoto wangu wote kwa wazaliwa wote wa kwanza kwenye madhabahu zozote ovu kwenye koo zetu kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, Amen

## SIKU YA 21: KUMFUNGUA NA KUMWEKA HURU MZALIWA WANGU WA KWANZA

Swala la kumwekwa huru mzaliwa wa kwanza kama tulivyosema kwenye kipengele cha maombi ya siku ya 20, kwamba wazaliwa wa kwanza wana vita kubwa sana kwa hiyo kama usipomfungua na kumweka huru kumwombea ni ngumu sana yeye mwenyewe kusimama kujiombea. Ni ngumu sana mfungwa kujitoa mwenyewe gerezani lazima waende watu wamtoe au wamfungue. Biblia inamzungumzia Petro alipokuwa gerezani

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

akiwa amefungwa na amewekwa katikati ya walinzi vikosi vya askari wanne wanne  wenye watu wamefungua minyororo ilibidi malaika aende gerezani mle ndio amfungue ile minyororo namgusa mwambie toka kwa hiyo ni ngumu sana mtu aliyefungwa kuweza kujiweka huru bila kufunguliwa. Ndiyo maana hata katika maisha ya kawaida mtu akiwekwa mahabusu lazima mtu aliyeko huru uraiani ndiye aende kumwekea dhamana atolewe, ndivyo ilivyo kwenye maisha ya ulimwengu wa roho kwamba ulimwengu tunaoishi tunahitaji neema ya kuwekwa huru.  Leo tunaenda kumweka huru mzaliwa wetu wa kwanza na kumwombea awekwe huru kweli kweli.

**Mistari ya maombi: Zaburi 113:5-8, Kumb.28:13, Ayubu 22:25 -28, Zab. 27:6, Hesabu 3:50-51**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Kazi ya kishetani inayoishika nyota ya mzaliwa wangu wa kwanza kwenye uzao wangu au kwenye familia yetu hiyo kazi iharibike na isimame tena kwa jina la Yesu Kristo
2. Baba katika jina la Yesu Kristo kila agano lolote la mababu zangu au mabibi walioliweka juu ya maisha ya wazaliwa wangu wa kwanza iwe wa kiroho wa kimwili hilo agano livunjike kwa jina la Yesu Kristo na wainuliwe waimarike kwa jina la Yesu Kristo
3. Katika jina la Yesu Kristo ninaivunja kila nguvu ya Herode wa kiroho wa ukoo wangu na familia yetu na taifa letu na kanisa letu ambayo imewafunga na kuwashikilia wazaliwa wa kwanza wasitoke kwenye hatma wasitoke au wavurugukiwe hatma zao katika jina la Yesu Kristo
4. Baba katika jina la Yesu Kristo ninavunja kila mipango yoyote ya kichawi iliyokusudiwa kubadili nyota yangu kama mzaliwa wa kwanza au nyota za watoto wangu wazaliwa wa kwanza au nyota za wazaliwa wote wa kwanza kwenye ukoo wangu hiyo mipango ya kichawi iteketekwa damu ya Yesu Kristo
5. Baba katika jina la Yesu Kristo kila laana na mapigo dhidi ya wazaliwa wa kwanza nyumbani mwa baba yangu au nyumbani mwa mama yangu hiyo laana ife na mzaliwa wetu wa kwanza awe huru kwa jina la Yesu Kristo
6. Baba katika jina la Yesu Kristo yeyote anayekwenda kwenye madhabahu za uovu na kufanya maagano au kutoa sadaka ili kuwafunga wazaliwa wetu wa kwanza kwa jina la Yesu Kristo

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

7. Ninawatoa na kuwakomboa wawe huru kwa jina la Yesu Kristo
8. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila kifungo kilichofungwa ufahamu na akili za wazaliwa wa kwanza kichawi hivyo vifungo vifunguke na vikatike vipande vipande na wawe huru kwa jina la Yesu Kristo
9. Baba kwa jina la Yesu Kristo ninamweka huru mzaliwa wangu wa kwanza na wazaliwa wote wa kwanza kwenye ukoo wetu na familia zetu wakiroho na wakimwili wawekwe huru kutoka kwenye mateso yoyote ya fikra na ufahamu katika jina la Yesu Kristo
10. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila kitambaa cheusi kilichofunga ufahamu na macho wasione fursa wazaliwa wa kwanza fursa ya elimu fursa ya biashara fursa ya kazi ya mafanikio ndio kitambaa tunakiteketeza kwa moto wa roho mtakatifu kwa jina la Yesu Kristo
11. Baba kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti kwa nguvu ya Mungu inayobadilika majira na nyakati ipambane dhidi ya lolote na madhara yoyote yanayowasifu wazaliwa wangu wa kwanza kwenye ukoo wetu kwenye familia au wazaliwa wa kwanza wa kiroho katika jina la Yesu Kristo hiyo nguvu iharibike na hiyo nguvu ya Mungu iwatoe kwenye mateso na kuwaweka kwenye maisha bora katika jina la Yesu Kristo

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

## SIKU YA 22: KUVUNJA NA KUHARIBU KILA MADHABAHU YA UOVU KWENYE FAMILIA NA KANISA LANGU.

Tunapozungumzia madhabahu tunazungumzia kitu kikubwa sana maana yake ni sehemu ambayo imetengwa maalum kwa ajili ya watu kukutana na Mungu, aidha Mungu wa miungu yao au Mungu wa mbinguni aliye hai aliyeziumba mbingu na nchi kwa lile eneo haliwezi huwezi kufanikiwa kama kuna madhabahu zaidi ya moja au zaidi ya mungu mkuu ambaye ni jumbe unaliomba mbingu na nchi na Bwana wetu Yesu kristo kama kuna vimadhabahu vyovyote kwenye familia ni ngumu sana kuweza kufanikiwa na hauwezi kujenga msingi wa madhabahu ya mungu aliye hai wa mbinguni kama hujavunja misingi ya madhabahu za ukoo ambazo zilitambikiwa na mababu na mabibi waliopita haijaishaunazifahamu au hauzifahamu na hii hali imeenda mbali zaidi kuna watu wengi sana tumejenga nyumba zetu juu ya madhabahu za miungu bila kujua umenunua kiwanja ukaikuta hicho kiwanja kumbe kuna mtu alikuwa anafanyaga pale matambiko au anafanyia vitu vibaya au wanafanyia maagano pale na wanafanya ibada zao za kuamini

sana au kuamini vitu vibaya na wewe unanunua hicho kiwanja unajenga nyumba yako mwisho wa siku unajikuta hali ya kiuchumi au maisha yanabadilika na kuna watu wengi sana wamenunua maeneo yakajenga nyumba magonjwa yakaanza kuwapiga ndani ya nyumba zao na wengine wakapoteza kazi na wengine wakaenda mbali wakafa kama tulivyomuona Naomi na mume wake ambaye alikuwa na watoto Wakilioni na Maroni unaona kwamba walitoka Benjamin ya Yuda wakaenda Moabu akafa kule, wakafa na watoto kwa sababu walitoka wakaingia kwenye hali ile ambayo ilikuwa ina madhabahu za miungu ya Moabu. Kwenye swala la kuvunja madhabahu za familia na kanisa ni lazima uombe maombi ya kumaanisha, maombi ya kina kuhakikisha unaondoa kila kitu.

**Mistari ya Maombi: Waamuzi 6:24-27, Daniel 11:32, Yeremiah 1:10, Hesabu 33:50-56**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Kwa jina la Yesu Kristo ewe madhabahu uliyenifunga mimi na familia yangu au ukafunga kanisa letu lisikue na kuongezeka ewe lango la kale ninaamuru moto kuteketeza na iteketeze madhabahu yako kwa jina la Yesu Kristo
2. Kila madhabahu ya familia nyumbani mwa baba yangu au nyumbani mwa mama yangu, wakwe zangu na waliokuwa wakwe zangu hiyo madhabahu ianguke na kuteketea kwa jina la Yesu Kristo
3. Madhabahu yoyote iliyosimamishwa dhidi ya maisha yangu, dhidi ya watoto wangu, familia yangu au dhidi ya kanisa langu au eneo la kanisa langu ili kutufanya tudhoofike hiyo madhabahu ivunjike na kuteketea kwa moto wa Roho Mtakatifu kwa jina la Yesu Kristo
4. Madhabahu yoyote iwe imejengwa chini ya maji iliyosimamishwa dhidi yangu na familia yangu au dhidi ya kizazi changu au imani yangu na kanisa langu, ili kuiharibu kazi ya mikono yangu hiyo madhabahu iteketee kwa jina la Yesu Kristo
5. Katika jina la Yesu Kristo madhabahu zozote za kichawi hizo simamishwa ili kupambana na wito wangu au kupambana na upako wangu wa kuinuliwa kwangu zisambaratike kuanzia sasa hivi kwa jina la Yesu Kristo Ee Bwana Yesu wewe uliye Bwana na mwokozi wa maisha yangu ninaenda kinyume na kila roho ya madhabahu yoyote hofu ambayo

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

imelitaja jina langu mahali popote ili usifanikiwe na kuongezeka hiyo madhabahu iteketee kwa jina la Yesu Kristo

6. Madhabahu zote za mababu nazozungumzia maisha yangu ili ni tende dhambi ili nisiishi maisha matakatifu hizo madhabahu kuanzia sasa ninakata mawasiliano na mteketee na kuvunjika kwa jina la Yesu Kristo
7. Ninavunja vunja kila madhabahu zote za uovu na kila madhabahu zote zinazotengeneza mauti kwenye kizazi changu familia yangu na kanisa langu kwa jina la Yesu Kristo
8. Katika jina la Yesu Kristo navunja madhabahu zote za uovu toka nilipokuwa nimezaliwa au nilipolelewa au nilipokuwa zamani kabla sijamjua mungu au zinazoandaliwa kwenye vizazi vyangu zote zivunjike kwa jina la Yesu Kristo
9. Baba katika jina la Yesu Kristo madhabahu zote zilizovunjika za waovu hazitajengwa tena na kuanzia sasa ninajenga madhabahu ya Bwana wangu Yesu Kristo kwenye vizazi vyangu vyote na kwenye kanisa langu na Yesu atawale na bendera yake naisimika ipepe usiku na mchana isishuke wala kuchanika katika jina la Yesu Kristo. Amen

## SIKU YA 23: HATIMA YANGU NA WATOTO WANGU PAMOJA NA KANISA LANGU LAZIMA ZIINULIWE JUU.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Hatima yangu na watoto wangu pamoja lazima ziinuliwe juu, maombi haya ya siku hii ni maombi ya kinabii ya kujitabiria na kujitamkia mema, wengi wetu tunajua kwamba kwenye maisha yetu wanaotutamkia mema ni wachache sana kuliko wanaotutamkia mabaya ingawa walioko upande wetu Katika roho ni wengi kuliko walioko upande wetu katika mwili.

kwa hiyo leo natamani unapoomba uombe kwa imani kubwa kwamba watoto wangu watainuliwa juu, kanisa langu litainuliwa juu ,mfano kanisa letu hili limepita wamepita watu wengi walioponywa na kufunguliwa lakini pia wengi wao baada ya kuponywa wamelinenea mabaya na kusahau yale matendo makuu ambayo Bwana aliwatendea jambo hili, sii jambo jipya liko wazi hata kwenye bibilia wakati wa Musa wana wa Israeli Musa alihangaika nao akawavusha mpaka jangwani lakini walipopata changamoto kidogo wakamnenea mabaya Musa hata kusema kwamba, kwa nini ulituleta huku tufe? maana kule kuona makaburi na wakakumbuka maisha yao ya misri ni sawa na kukumbuka maisha yako ya duniani kwamba kule nilikuwa nakula

matikiti maji na nyama na kusahau hatima kubwa na nguvu kubwa aliyoifanya Musa.

Ndicho kinachoendelea hata kizazi hiki kwamba tulio wengi tunaweza Mungu akatuinua akatufungua lakini baada ya kuwa tumepona ikitokea makwazo kidogo huwa tunanena mabaya juu ya mahali tulipokuwa tumefunguliwa kama kwa maana ya kanisa au hata watoto wa watu wale ambao tulikuwa msaada kwetu.

leo unapoomba, omba mema watoto wako kwamba watainuliwa juu ,tamkia mema kanisa lako kwa watainuliwa juu katika jina la Yesu Kristo.

**Mistari ya maombi: Warumi 12 :2, 1 Wakorinto 15:13,18-19, 1 Thes 4:3, Luka 2 :52**

**Vipengele vya maombi**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo naitenga familia yangu na marafiki na rafiki yeyote ambaye atawaweka watoto wangu na kizazi changu mbali na Mungu kwa jina la Yesu Kristo.
2. Baba kwa jina la Yesu Kristo nawaweka mbali watoto wangu na vizazi vyangu vyote wakae mbali na mambo maovu na ubaya wote wa dunia hii bali wainuliwe katika kumjua Mungu na Yesu Kristo kwa jina la Yesu Kristo.
3. Baba kwa jina la Yesu nakata mizizi yote ya tamaa mbaya za kishetani kwa watoto wangu, uasherati dhambi ya ngono upotovu wa mali kutoka katika maisha ya watoto wangu na vizazi vyangu na ndani ya kanisa bali natamka wainuliwe juu katika kumjua mungu katika jina la Yesu Kristo
4. Baba katika jina la Yesu Kristo natamka na kuamuru kuwa watoto wangu watakuwa ni watoto wenye kuheshimu wazazi wao, kuwaheshimu kila mtu watakayekutana naye na watumishi wa mungu bali hawataingia katika mkumbo wa masengenyo na kukosoa katika jina la Yesu Kristo.
5. Ee bwana Yesu wainue wanangu na binti zangu inua hatima zao na vizazi vyao na uwakabidhi funguo za mataifa kila watakapoingia katika taifa lolote wawe juu tu wasiwe chini kwa jina la Yesu Kristo
6. Mungu wa Eliya ujibuye kwa moto natamka kwamba Roho Mtakatifu unayemwaga vipawa kwa vijana na nguvu kuliko uasi na mabaya yote,

haleluya.tv Changing the World from Pain to Praise

natamka vipawa kwa vijana wa kanisa na nguvu kwa watu wote na watoto wao ndani ya kanisa hili kwa jina la Yesu Kristo.

7. Ee Bwana Yesu, wewe ni mpigania uhuru mkuu, natamka kwa jina la Yesu Kristo, Kila mtoto wa madhabahu hii au watoto wetu kwenye vizazi vyetu wapokee uhuru kutoka kwenye mikono ya adui katika jina la Yesu Kristo.
8. Baba katika jina la Yesu natangaza na kutamka uhuru dhidi ya watoto wetu na vizazi vyao na kanisa hili hawatatumikia nguvu za giza wanakumalizia kwenye mwisho mbaya katika jina la Yesu Kristo.
9. kwa mamlaka ya jina la Yesu kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu ya watoto wa kanisa hili na madhabahu hii na watoto wetu wote watapewa kuteka na kumiliki na majina yao yatatajwa vinywaji vya kuwa nje na wafalme katika jina la Yesu Kristo.
10. Mungu wa haki na nguvu inua hapa kwa mafuta watakaoongoza katika njia ya haki nguvu ya roho na maarifa miujiza na matendo makuu katika kanisa hili sawasawa na kitabu cha luka 4:19 na isaya 61:1-2 katika jina la Yesu Kristo.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 24: KUSHUGHULIKA NA ROHO YA YEZEBELI NA KUMWANGUSHA ANAYEPAMBANA NA KANISA NA MAISHA YANGU.**

Wengi wanasikia Yezebeli Yesu, ni roho inayoongelea kwa habari ya uongo mchawi , kwa maana ya unabii wa uongo ,uchawi , Ushirikina, uzinzi ,washerati na mambo hayo yote machafu ,ukahaba na kila namna, hii ni roho ambayo inafanya kazi kwenye familia zetu zilizo nyingi ,kwa nini? kwa sababu unakuta kati ya watu watano, watatu unakuta wanaenda kwa waganga ,wengine wanaachiliwa roho za ukahaba uzinzi washerati na mambo kama haya lakini pia inafanya kazi sana ndani ya kanisa hasa kwenye umri wetu, vijana wetu wa kanisani kwenye makundi kama ya kwaya, makundi mbalimbali hata kwenye watu wa maombi ,mmoja anaingiliwa na ile roho ya Yezebeli inaanza kubadilika kwenye ndoto na kutoa unabii wa uongo na kadhalika ,imepiga sana makanisa yenye nguvu, tunamuona kama Eliya alivyokuwa nabii mwenye nguvu alishusha moto lakini cha ajabu Yezebeli tu ,tena mwanamke na mabinti zake walivuruga ufahamu wa Eliya na maono yake mpaka akaomba kufa, kwa hiyo tunaposema roho ya Yezebeli sii roho tu ndogo au kitu cha kawaida ,ni kitu kikubwa sana

kinachofanya kazi kwa viwango vikubwa vya nguvu za kishetani au nguvu za ufalme wa giza kwa hiyo unapoomba haya ni maombi ya vita ya hatari sana ambayo unatakiwa kuyaomba kwa mzigo kutoka ndani katika jina la Yesu Kristo, amen.

**Mistari ya maombi: 1 Wafalme 19:1-3, Ufunuo 2:18-21, Mika 5:10-12**

**Vipengele vya maombi**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo na Mungu mwenye nguvu ushushaye moto, nashusha moto dhidi ya roho yeyote ya Yezebeli inayofanya kazi ndani ya familia yangu au kwenye familia ya watu wetu na jamaa zangu au ndani ya kanisa, roho ya Yezebeli inayonawaingiza watu kwenye uzinzi na kuwatisha iteketee kwa jina la yesu Kristo.
2. baba kwa jina la Yesu nakemea kila roho zozote za mafundisho ya uongo ,unabii wa uongo ,ibada za sanamu na uovu wowote unaohusiana na Yezebeli ndani ya kanisa ndani ya familia katika jina la Yesu Kristo.
3. Baba kwa jina la Yesu Kristo ninakataa kila nia ovu ya Yezebeli ambayo ina mabinti zake inayolivuruga kanisa na kuvuruga vijana na kuvuruga vikundi mbali mbali vya kanisa vya maombi, waimbaji na wengineo ili wasiwe na moto wa Roho Mtakatifu na kusoma neno katika jina la Yesu Kristo
4. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti navunja nguvu na kila neno lililotoka kwa Yezebeli dhidi ya maisha yangu na maisha ya watu wangu na maisha ya kanisa langu ambayo inasababisha watu wadhoofike kiroho katika jina la Yesu Kristo.
5. Kwa jina la Yesu Kristo najitenga na laana zote za Yezebeli na roho zake zinazofanya kazi katika ukoo wangu au watoto wangu na ndani ya kanisa najitenga na laana zote alizotamka kutoka kinywani mwake katika jina la Yesu Kristo.
6. Kwa jina la Yesu Kristo ninakemea na kufutilia mbali kila ukahaba na uchawi ambao umeingizwa na uchawi wa Yezebeli ambao umeingizwa ndani ya familia zetu au ndani ya kanisa letu ,hizo nguvu zake zivunjike maishani mwetu kwa jina la Yesu Kristo
7. Namkemia Yezebel na kumkatakata vipande vipande na mabinti zake, na nguvu zake na uchawi wake wote ambao unafanya kazi katika kizazi hiki cha sasa na katika kanisa la sasa ulimwenguni kote ili kuuwawa na

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

kuangamiza watu wasipende kumtafuta mungu kwa bidii katika jina la Yesu Kristo.

8. Baba katika jina la Yesu ninakemea na kuzifunga roho zote za kichawi tamaa mbaya vishawishi vitisho ibada za sanamu ukahaba zinazohusiana na Yezebeli kwenye kanisa au familia zetu kwa jina la Yesu Kristo
9. Naamuru Yezebeli na kizazi chake chote na wote anawafundisha uchawi wake na uganga wake na mabinti zake waangushwe chini na wasiinuke tena katika jina la Yesu Kristo.
10. Baba ninaachilia ulinzi wa damu ya Yesu Kristo wa Nazareti tunazungushia ukuta wa moto ndani ya familia zetu na kanisa letu Yezebeli asiweze kupenyesha tena silaha zake katika jina la Yesu Kristo.

**SIKU YA 25: KANISA LANGU LAZIMA LISONGE MBELE KWA NGUVU KUBWA YA USHINDI**

kusonga mbele kwa kanisa au jambo lolote kunategemea nguvu ya kiroho ndio maana hata Yesu alisema katika kitabu cha, Yohana 17:15, kwamba siwaombei mtolee ulimwenguni bali nawaombea mshinde ule ulimwengu na kumshinda yule muovu, kwa hiyo kama kanisa la kiroho ili linuke juu zaidi tunahitaji kuomba kwamba kwenye huu ulimwengu uliojaa vita ,mashindano na nguvu za yule muovu shetani ,Yesu atupe nguvu ya kuushinda ule uovu ili tuinuke juu .

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

Kwenye maombi haya omba kabisa kwamba Mungu akupe nguvu ya kushinda yule muovu si kututoa ulimwenguni na haya ni maombi ya vita kwamba mungu atupe nguvu ya kumshinda yule muovu ,ili kuinuka hauwezi kuushinda uovu au kumshinda shetani kama hauna nguvu ya Yesu Kristo ndani yako .

**Mistari ya maombi: Mathayo 9:35-38, Wakolosai 1:9-11, Yohana 17:15, Thes. 1 :11-12**

**Vipengele vya maombi**

1. kila roho yoyote ambayo inasababisha kwamba muovu atushinda kwenye ulimwengu tunaishinda kwa damu ya Yesu na tunainuka jua tutakuwa chini tena katika jina la Yesu Kristo.

2. kwa mamlaka ya jina la Yesu Kristo ninakanyaga na kuua kila joka yeyote ambaye anaharibu na kula yale matunda ya kanisa ili isiinuke huyo joka tunamponda kichwa na kumharibu kwa jina la Yesu Kristo.
3. Naamuru kwa jina la Yesu Kristo, kila mlima ulio mbele ya ukuu wa jina la kanisa hili jina lisiinuke na kanisa lisiinuke kusimama juu ya kilele cha mlima huo mlima ubomolewe kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti.
4. Bwana wetu Yesu Kristo, kwa maana imeandikwa mavuno ni mengi ila watendakazi ni wachache na ninatuma malaika wa mbinguni waende kwenye kila kona na mahali kokote ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania kuwaleta watenda kazi kwa ajili ya mavuno kwa kuwa shamba li tayari katika jina la Yesu Kristo.
5. Baba katika jina la Yesu Kristo nafungulia ulinzi wa kimbingu dhidi ya mipango ,mapigano ya kishetani ambayo yanapiganwa na kuvunja na kushusha nguvu ya Mungu ndani ya kanisa letu ya ufanisi katika jina la Yesu Kristo .
6. Bwana Yesu simamisha ngao kuzunguka kanisa letu la omega kwa nguvu ya damu ya Yesu nalisimamiwe tena wale watu wake kuvamiwa kwa jina la Yesu Kristo, Roho Mtakatifu wewe udhihirishaye nguvu za kimungu dhilisha na kuharibu ngome zote ndani ya kanisa la omega nazozuia uamusho wa injili, miujiza ,matendo makuu ya kimungu badala yake kumpa shetani fursa ya ya ukosoaji na kiburi na majivuno hizo roho zote ziteketee kwa jina la Yesu Kristo.
7. Baba katika jina la yesu kristo anza kulisimamia mwenyewe kundi la maombi, kikundi cha maombi ili kuwafanya wana maombi na walinzi wa kanisa kuimarika kiroho na kufungua macho yao kupata mafunuo ya kutenda mambo makubwa kwenye maombi katika jina la Yesu Kristo.
8. Bwana Yesu kwa jina lako takatifu tunainuka juu kama kanisa kupita roho yoyote ya mababu waasisi wa injili kwenye nchi, kanisa letu la omega litainuka juu na halitashuka chini.
9. Katika jina la Yesu Kristo, nguvu yoyote inayofanya kazi kwenye taifa hili ili kuyafanya makanisa ya dhoofike ya kose nguvu ya Mungu mpaka mwisho hiyo nguvu tunaidhoofisha na kujua kwa jina la Yesu Kristo.
10. Kila aina ya uchawi wowote unaotumika kuiangusha makanisa kuangusha watumishi wake katika taifa hili kanisa la Omega halitaanguka kamwe chini bali litainuka juu katika jina la baba katika jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**SIKU YA 26: KUSHUGHULIKA NA KUIUWA KABISA ROHO YA BADO KIDOGO**

Hii roho ya bado kidogo ni roho mbaya sana,inaua maono, inaharibu muda ,inaharibu utaratibu ,mipango na kila aina ya namna ya maisha . Watu wengi sana wanapoona dalili za mafanikio wanafikiri tayari .Roho ya bado kidogo inaua mtazamo wako wa maombi, nguvu ya kuamka kuomba, kwa sababu unajua vitu vimekaribia, inakuonyesha ishara na haikuonyeshi muujiza, ni roho iliwatesa wana waIsrael walikuwa wanaambiwa watafika Kanani kwa muda wa siku tatu ,lakini walikaa karibu miaka 400 kwa sababu walionyeshwa ni pale lakini hawafiki ,asilimia kubwa katika uchunguzi wangu na kazi hii inayofanya kwa miaka hii tangu nimeanza nimegundua tulio wengi tunateswa na hii roho kuliko roho yoyote .

Inaweza ikakuletea muujiza ukaona ishara na dalili zaidi ya mwaka, unakaa unasubiria kitu na hakitokei na unapunguza kasi ya maombi ,nakushauri usiache kuomba mpaka umeushika muujiza wako mkononi , walipoona mapigo yameongezeka na kuwapiga na kuharibu, Wana wa Israeli, Musa akapigana na Farao alipoona mapigo yamekuwa makubwa ,akasema mwende lakini msiende mbali, kwenye kitabu kile cha kutoka , huu ni mstari mkubwa wa kusimamia ,kitabu cha Kutoka,biblia inasema akaufanya tena moyo wake kuwa mgumu na asiwape ruhusa tena ,ndivyo ambavyo shetani anafanya kazi anapoona umekaa kwenye mfungo unaomba ,unapiga maombi ,shetani huwa  ana kanuni ya kukuacha kidogo au anakuonyesha ishara fulani zinaanza kutokea kama za upenyo mafanikio baadaye ukipoa anarudisha pale pale vifungo vyake na anaongeza zaidi kwa hiyo roho ya bado kidogo lazima uipige kwa nguvu sana katika jina la Yesu Kristo ,Amen.

**Mistari ya maombi: Kumb.32:48-52, 2 Wafalme 5:1 -15, 1 Thes 4 :16 -17, Zab 138 :8**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba kwa jina la Yesu Kristo kila roho ya uzito ya farao ambayo inanipa ruhusa niende ila nisiende mbali kwenye ukoo, kwenye familia na vizazi vyangu kwenye jamii yangu naipiga na kuisambaratisha iniachie niondoke jumla na nifanikiwe kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise

2. Kila chungu cha uchawi kinachochemka ili matatizo yangu yaendelee kuwepo kila siku maishani mwangu kwa jina la Yesu Kristo, kila chungu cha kichawi na madhabahu yoyote ya kichawi kinachohifadhi heshima na utu wangu hicho chungu kivunjike na heshima yangu iachiliwe jumla kwa jina la Yesu Kristo.
3. Baba kwa jina la Yesu Kristo nguvu ya bado kidogo inayofanya kazi maishani mwangu ili nisifanikiwe jumla, nisipate muujiza wa kudumu, hiyo nguvu ikauke kwa moto wa Roho Mtakatifu kwa jina la Yesu Kristo.
4. Baba kwa jina la Yesu Kristo napasua na kusambaratisha kila njia yoyote ya watesi wanaotesa maisha yangu na nikiomba wanaachia kwa muda cheo change, nikitulia wanakishikilia cheo changu hiyo nguvu ya kishetani inayonizuia nisipandishwe au nisipate muujiza kupitia watesi hiyo nguvu iteketee na kuharibika kwa jina la Yesu Kristo.
5. kila maneno yoyote yalinitamkia mabaya laana inayonizuia nisiende mbali, nikae mahali pamoja ili nisisonge mbele, hayo maneno nayafuta na huyo matamko, hayo maneno iwe ni ufalme wa giza na mapepo yake yafe na kuteketea kwa jina la Yesu Kristo.
6. Nguvu zote za mashetani zinazonifuata ili nisifanikiwe maishani mwangu hizo roho iwe zinakaa milimani, baharini, njia panda, kwenye koo zetu au mahali popote hizo roho zife na sizisiinuke tena kunifuata kwa jina la Yesu Kristo.
7. Baba kwa jina la Yesu Kristo, mlima wowote wa upinzani uliosimamishwa na mababu zangu au bibi zangu kwamba hawa watu hawatafanikiwa zaidi ya sisi tuliokufa, huo mlima usambaratike na maneno yao yafutike kwa jina la Yesu Kristo
8. Baba kwa jina la Yesu Kristo ukuta wowote wa kishetani uliojengwa mbele yangu ambao unasema sitaweza kuvuka kiwango fulani cha baraka au mafanikio au maisha, huo ukuta uvunjike na hautajengwa tena katika jina la Yesu Kristo.
9. Baba kwa jina la Yesu Kristo, roho ya bado kidogo haitanishikilia tena na ninapotoka haitanifuata tena, nitafanikiwa kuliko mababu zangu na mabibi zangu na mtu yeyote kwenye ukoo wangu hakuna atakae nipita mimi na kunishinda katika jina la Yesu Kristo.

**SIKU YA 27: NIMEBARIKIWA NA BARAKA ZANGU HAZITAJIFICHA WALA KUFICHWA TENA KATIKA JINA LA YESU KRISTO**

Maombi haya tunapoelekea siku za mwisho kumalizia au tunapoelekea tamati kumaliza siku za maombi yetu lazima ukiri kwa kinabii baada ya kuachiliwa kutoka kwenye roho ya bado kidogo, sasa jua kabisa umebarikiwa na baraka zako hazitajificha, watu wataziona na baraka zako zitawavuta watu kuja kwa Yesu kwa utukufu wa jina la Yesu Kristo, sio kwa ajili yako .Kwa hiyo utakapobarikiwa usijivune kwa sababu tumebarikiwa kwa ajili ya Kristo, tumebarikiwa kwa ajili ya kuinua jina lake, tumebarikiwa ili wengine watakapoona wasioamini wapate kuamini na kumfuata Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yao.

kwa hiyo unapokiri maombi haya kama alivyosema kwenye kitabu cha kumbukumbu la torati 28 :2 na kuendelea, kwamba nitabarikiwa mashambani, nitabarikiwa mjini nitabarikiwa niIngiapo, nitabarikiwa niKitoka, hapo itabarikiwa chupa ya mafuta, litabarikiwa kapu langu la unga ,ndivyo ambapo kila mahali utakapoenda utakuwa baraka na utakuwa rahana. Kitabu cha Waefeso, mtume paulo anawaandikia watu waefeso 3: 20, "atukuzwe Mungu Baba awezaye kufanya mambo makubwa mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo kadri ya nguvu ile itendayo kazi ndani yetu",ndivyo itakavyokuwa kwenye maisha yako kwamba yale uliyoyaomba miaka mingi iliyopita mwaka huu baraka zitaonekana pasipo kujificha kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Mistari ya maombi: Isaya 55:5, Da. 6 :18-22, 1Sam 1:1-6, kumb. 28:1-13**

**Vipengele vya Maombi:**

1. Nimebarikiwa, nina wimbo mpya, mafuta mapya, katika jina la Yesu.
2. Baraka zangu hazitajificha mwaka huu kwa jina la yesu kristo.
3. Nimebarikiwa napokea maji ya uhai ili nipande juu zaidi na mafanikio yangu hayatajificha kwa utukufu wa Bwana wangu Yesu Kristo.
4. Nimebarikiwa kama alivyosema Mungu nina ndoto kubwa na matarajio makubwa mungu wa mbinguni misimamie niwe juu tu nisiwe chini na baraka zangu zisijifiche katika jina la Yesu Kristo

5. Baba kwa jina la Yesu Kristo nguvu yoyote inayozuia baraka yangu kutokea kijijini huko nilikozaliwa au kulelewa inayofuatilia zisionekane, ninaamuru kwa moto wa Roho Mtakatifu hiyo nguvu isinifuate tena katika jina la Yesu Kristo.
6. Kwa mamlaka niliyopewa na Yesu Kristo naamuru kila lango ovu lililojengwa ili kuzuia hatima yangu ising'ae ishike moto sasa hivi kwa jina la Yesu Kristo.
7. Baba kwa jina la Yesu Kristo mawakala wote wa kuzimu wanaoshindana na kutumwa kufuatilia baraka zangu, waliopewa kazi dhidi ya maisha yangu ili wanifuatilie wanizunguke nisipige hatua, hao mawakala wote washikwe wazimu na kuchanganyikiwa kwa jina la Yesu Kristo.
8. Kila macho ya watesi yanayonitafuta na kunifuatilia na kunitazama kwamba mtu huyu hatokabarikiwa na baraka zake hazitaonekana, macho yao nayatoboa kwa misumari ya moto kwa jina la Yesu Kristo.
9. Baba kwa jina la Yesu Kristo nakataa kila mpango wa kushushwa cheo kushushwa kihuduma kiupako, kimafanikio, kwenye kila nyanja ya maisha yangu huo mpango usambaratike kwa jina la Yesu Kristo
10. Baba kwa jina la Yesu Kristo nakataa kufa kama watu wengine waliokufa bila kuona matokeo na mafanikio yao kwenye familia, mimi sitakufa bali nitaishi katika jina la yesu kristo.
11. Kwa jina la Yesu Kristo, natangaza kuvuruga makao makuu ya nguvu za giza, nguvu za wachawi zinazopambana kugeuza jina langu lisijulikane nisitambulike, nisitajwe, hayo makao makuu yao nayapiga bomu la kiroho katika jina la Yesu Kristo.
12. Baba kwa jina la Yesu Kristo nafungulia radi isiyokuwa na kikomo wala mwisho kwenye kona yoyote ya mtu au mnyama, mzimu au mwanadamu madhabahu au uchawi haijalishi yeye ni nani ana jina gani yeyote anayesimama baraka zangu zisionekane nafungulia radi ipige na kupasua pasua kwa jina la Yesu Kristo.
13. Baba katika jina la Yesu Kristo kila chungu chochote cha kichawi kwenye maisha yangu kilichokuwa kinazuia baraka zangu zisionekane

zitambulike kama Yesu alivyofufuka akashinda mauti na akatoka kuzimu, hicho chungu nakipasua na ninatoka nje na baraka zangu zionekane kwa jina la Yesu Kristo, Amen.

**SIKU YA 28: NIMEFUNGULIWA NA NIMEACHILIWA ILI NISHINDE KWA JINA LA YESU KRISTO.**

Kwa awamu hii ya maombi ya mwisho tumeachiliwa ili tushinde, kama ambavyo neno la mungu linasema kwenye kitabu cha warumi 8:1, Sasa basi , hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu,hivyo basi sisi hatuna tena hukumu yoyote ya adhabu kwa sababu tuko ndani ya kristo yesu .Mwaka huu utakuwa wa ushindi na zaidi ya kushinda, bendera ya Yesu Kristo, Bwana na mwokozi wa maisha yetu lazima itapepea ,kwa hiyo unapoomba ombi hili jitamkie kwamba mimi umeachiliwa ili ushinde kwa jina la Yesu Kristo.

**Mistari ya maombi: Mathayo 13:24 -30, 2wafalme 5:20-27, Warumi 8:3-6, Danieli 6:16-23**

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**Vipengele vya Maombi:**

1. Baba katika jina la Yesu Kristo, muweza wa yote na mwenye mamlaka kuliko vyote, chochote kile ndani yangu kinachopunguza kasi yangu ya ushindi isiinuke juu kiteketee kwa moto wa Roho Mtakatifu .
2. Baba katika jina la Yesu Kristo, kama kuna mtu yoyote au mnyororo wowote unaonifunga ili nisisonge mbele kwa mambo makubwa, hiyo kamba iniachilie na hiyo minyororo ikatike kwa jina la Yesu Kristo.
3. Kila mbegu ya kishetani ndani yangu inayozaa matunda ya kushindwa ili nisishinde maishani mwangu, hiyo mbegu ifie huko huko na iteketee kwa moto wa Roho Mtakatifu kwa jina la Yesu Kristo.
4. Baba katika jina la Yesu Kristo mpango wowote wa maadui zangu dhidi ya hatima yangu nzuri na mafanikio yangu ya ushindi makubwa hiyo mipango ivunjike katika jina la Yesu Kristo.

5. Baba katika jina la Yesu Kristo, nautupa motoni ulimi wa mtesi yeyote, huo ulimi unaonitamkia mabaya kwamba sitashinda nitakufa lini jina langu lipotee, huyo mtesi na ulimi wake nautupa kwenye moto kama vile ulimi wa joka mwenye ndimi za fira katika jina la Yesu Kristo.
6. Baba kwa jina la Yesu Kristo yeyote aliyekopesha maisha yangu kwa agano la uovu na maagano yake yakanifunga nisiweze kupata ushindi na kufanikiwa nayakataa na ninajikomboa maisha yangu kutoka kwenye deni la uovu kupitia damu ya Yesu Kristo.
7. Baba kwa jina la Yesu Kristo nguvu yoyote mtaani kwangu ninakoishi au nilipozaliwa,nilikolelewa, upande wa baba yangu au mama yangu ambayo inazuia ushindi wangu au inauchelewesha, hiyo nguvu iteketee na ninaichoma na kuiangamiza kwa moto wa radi kwa jina la Yesu Kristo.
8. Baba kwa jina la yesu Kristo yeyote aliyeiba funguo zangu za ukuu, ushindi na mafanikio muda wako umeisha, rudisha funguo zangu zote na nishinde zaidi ya kushinda kwa jina la Yesu Kristo.
9. Baba kwa jina la Yesu Kristo popote pale ambapo vipaji vyangu na uwezo wangu umetawanywa au umechukuliwa ninapavuruga na kupateketeza kwa jina la Yesu Kristo.

haleluya.tv
Changing the World from Pain to Praise

**HATUA INAYOFUATA BAADA YA KUMALIZA MFUNGO WA SIKU 28**

1. JUU YA KUKIRI USHINDI NA KUSHINDA

2. KUTOKUKUBALI KURUDI ULIPOTOKA WALA KUWAZA.

3. NAMNA YA UTOAJI WA SADAKA ZETU ZA MALIMBUKO KWENYE IBADA YETU KUBWA YA KIHISTORIA ISIYOSAHAULIKA KWENYE MAISHA YETU YA MKESHA WA USIKU WA 2/2/2025 "USIKU WA MALIMBUKO YANGU NA MIUJIZA YA KUPITA KAWAIDA"

haleluya tv
Changing the World from Pain to Praise